# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TANO

### Kikao cha Nane – Tarehe 11 Novemba, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Tano, leo ni Kikao cha Nane. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Hati za Kuwasilisha Mezani.

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.6) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2021].*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikaili. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Tarimba Abbas.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 6) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2021].*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba, tunakushukuru. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuomba sasa usonge hapo mbele. Ahsante sana. *(Makofi)*

Naomba nimwite mwuliza swali wa kwanza, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya. Hayupo. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, uliza swali lake.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nami kupata nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, magonjwa yasiyoambukiza; *cancer,* moyo na figo, yamekuwa yakitesa sana wananchi na yana gharama kubwa sana: Je, ni lini Serikali itaamua kuleta ile Bima ya Afya kwa wote ili kupunguza maumivu makubwa ambayo yanawapata kwa sababu gharama ni kubwa sana? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakagenda, Mbunge wa Mkoa wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba magonjwa haya sasa hivi nchini yamekuwa yanasumbua sana; *cancer,*

magonjwa ya moyo, figo, pia hata *BP,* kisukari, ni miongoni mwa magonjwa ambayo Serikali kwa sasa imeyawekea msisitizo na mkazo kwamba yapewe kipaumbele katika kutoa tiba. Ndiyo maana kwenye sera yetu magonjwa haya kwenye maeneo mengi yanatolewa bure ili mgonjwa anapopata tatizo hili aweze kutibiwa bila gharama zozote.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mchakato wa kukamilisha kuanza kwa Bima ya Afya kwa Wote. Tayari hatua za awali mpaka Baraza la Mawaziri imeshapitishwa; uko upungufu kidogo unatakiwa uimarishwe. Kwa sababu tunazungumzia Bima ya Afya kwa Wote, tunaendelea kupata uzoefu na ushauri na wadau kwa sababu Serikali ilianza na Bima ya Afya ile ya jamii inaitwa *CHF;* yako mafanikio na pia upo upungufu. Pia, tukawa na Bima ya Afya ya wafanyakazi *NHIF* ambayo pia nayo tumepata mafanikio, lakini pia changamoto zipo.

Mheshimiwa Spika, tunapokuja kuzungumzia Bima ya Afya kwa Wote sasa tunaanza kupata ule uzoefu tulioupata kwenye *CHF* na *NHIF* ili tuone namna ambavyo tutapanua na kumfikia kila Mtanzania, kila mmoja kwa pembe zote nchini ili tunapoanza Bima ya Afya tusiwe na upungufu mwingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo hatua ambayo Wizara ya Afya inaendelea nayo kwa kushirikiana wadau, wale ambao wanatoa Bima ya Afya kwenye taasisi mbalimbali nao; hizi taasisi za bima ya kawaida ambapo pia nao wanatoa huduma ya matibabu ili tuweze kuweka utaratibu ambao utatufikisha. Kwa hiyo, Serikali sasa ikishakamilisha magonjwa hay ana wenzetu ambao wanapata tatizo hili tutakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuhudumiwa. Kwa hiyo, nawaomba sana Watanzania mtuvumilie.

Mheshimiwa Spika, pia, Bunge letu tunaliomba lituvumilie, tukamilishe eneo hili ili tutakapokuwa tunaleta Bungeni tayari kwa kuanza, tuanze tukiwa tuna uhakika kwamba hatutakuwa na upungufu mwingi. Hiyo, ndiyo

dhamira ya Serikali na tukishakamilisha hilo Muswada ule utaletwa hapa, utapitiwa na Waheshimiwa Wabunge ili tupate sasa mawazo yenu, mchango wenu na maoni yenu ya mwisho halafu tuidhinishe sasa Bima ya Afya kwa Wote iweze kuanza. Huo ndio utaratibu wa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Longido, Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, uliza swali lako.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kumwuliza Waziri Mkuu swali. Kwa kuwa lengo la Sera ya Manejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, ilitengenezwa toleo la pili mwaka 2008 ili kuboresha utumishi wa Umma na huduma zinazotolewa na Serikali kupitia watendaji wake kwa kuzingatia sifa na usimamizi unaotoa mwelekeo: Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu...

**SPIKA:** Mheshimiwa naona kuna karatasi hapo mbele, kama vile unasoma. Hebu mwangalie Waziri Mkuu, halafu uliza swali.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuwa nataka kunukuu lengo la Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ambao unasisitiza kwamba watumishi wanaoajiriwa ni wale wenye sifa na ndio watakaosimamia matokeo tunayohitaji katika utendaji wa Serikali.

Na kwa kuwa tuna watumishi wengi wenye sifa katika ngazi ya kada za Watendaji wa Vijiji ambao wamefanya kazi hiyo kwa kujitolea kwa miaka mingi na kumekuwa na tatizo la kutoa vibali vya kuajiri:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaajiri ili kuondoa hiyo kero ya hawa watumishi ambao hawana ufanisi kwa sababu ni...

**SPIKA:** Ahsante sana. Umeeleweka Mheshimiwa. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulianzisha mfumo ambao unaweza kuwafikia Watanzania wote katika kuajiri badala ya kuziachia sekta ambazo zilikuwa zinaajiri au kwa upendeleo au kwa namna ambayo wengi walikuwa wanalalamikia. Kwa kuunda Tume ya Ajira, tunakusanya nafasi kwenye taasisi zote zinazoombwa, tunaziombea kibali kwenye mamlaka. Tukishatoa kibali, Tume yetu inatoa tangazo Watanzania wanapata nafasi ya kuomba na kuitwa kwa ajili ya usaili halafu wanaweza sasa kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, hawa ambao wanafanya kazi kwa kujitolea kwenye maeneo yetu ya vijiji, kata na pia kwenye Halmashauri zetu wapo kwenye sekta kama afya na elimu, tunao. Wale wote ambao wanafanya kazi kwa weledi na wana sifa ya kuajiriwa, pindi tunapopata vibali kutoka Utumishi, tunawaajiri. Sasa hivi tumeshatoa maelekezo kwenye Halmashauri, wako vijana ambao wanafanya kazi kwenye Halmashauri zetu kwenye nafasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya elimu wako walimu wanajitolea na wana nafasi nzuri; kwenye kata, pale kwenye mapengo tunao vijana kwenye vijiji vile, wanafanya kazi yao vizuri. Hawa wote tunaendelea kuwaangalia na kukusanya taarifa zao na sifa zao. Inapotokea kuwa na vibali ambapo sasa vinaendelea kuzalishwa kuajiri kada mbalimbali, itakapofikia kwenye kada hiyo, nao pia tunawapa nafasi ya kuwaajiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inaendelea kuwaangalia hawa wote ambao wamejitoa, wameamua kufanya kazi bila mshahara, lakini pia wanataka kuonesha uwezo wao na kuutumia muda wao vizuri kulisaidia na kulihudumia Taifa hili, wote wanapata kipaumbele kwenye ajira.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie wale wote ambao wanajitolea, tulikuwa tunazungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi

ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, juu ya vijana wetu ambao wanafanya kazi kwa kujitolea kule kwamba, hawa sasa waorodheshwe tuwatambue ili baadaye ajira inapotokea, waweze pia kuingia kwenye orodha ya waajiriwa. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu ambao tunautumia kwa sasa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, uliza swali lako.

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali imekuwa ikiwekeza fedha nyingi katika miradi ya ujenzi wa meli katika maziwa makubwa yaliyoko nchini mwetu likiwemo Ziwa Viktoria, Nyasa na sasa Tanganyika. Hata hivyo kumekuwa na ufanisi mdogo sana katika kutoa huduma kutumia meli hizo katika maziwa hayo:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kuwa meli hizi zilizojengwa kwa gharama kubwa zinatumika ipasavyo ikiwemo katika Ziwa Nyasa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mbunge wa Mbambabay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeimarisha sana huduma za usafiri kwenye kada zote, maeneo yote ya barabara, hewani, kwenye maji, lakini pia kwa njia ya reli. Kama ambavyo Watanzania mnajua, miradi kadhaa inaendelea ikiwemo na utengenezaji wa meli ambazo zinatoa huduma kwenye maziwa yetu na ukanda wa bahari ikiwemo na Ziwa Nyasa; na kwa bahati nzuri nimepata nafasi ya kwenda Nyasa na kuzindua meli kadhaa:-

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge anaomba kujua utoaji huduma wenye tija; ni swali pana kidogo.

Mheshimiwa Spika, utoaji huduma wenye tija, mkakati wetu ndani ya Serikali, kwanza ni kupanua wigo wa kufanya biashara hiyo na kwa kuwahudumia Watanzania. Hii ina maana ya kwamba, kama tuna vituo vichache vinavyolazimisha wananchi walioko mbali kufuata bandari, lakini kwenye maeneo walimo, tunaweza kujenga bandari. Ndiyo mkakati ambao sasa unafanywa na Mamlaka ya Bandari kwa kujenga bandari palipo na watu wengi ili kuweza kuwafikia ili huduma sasa iwe na tija. Hiyo ni moja.

Mheshimiwa Spika, pili, sisi tunafanya kazi kule Ziwa Nyasa na nchi ya Malawi. Nchi ya Malawi ni ndefu kufuata lile ziwa, lakini tuna bandari moja tu ya upande wa Malawi. Sasa ili kufanya huduma hizi ziwe zenye tija, nako pia kushawishi kuwa na bandari nyingine ili tuweze kuwapata abiria wengi ili na yenyewe iweze kuwafikia Watanzania kwenye huduma hii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tunataka tuimarishe ratiba za meli ziwe mara nyingi zaidi kuliko ratiba ambayo inawafikia wananchi mara chache. Labda kama ratiba hiyo ni mara moja kwa wiki, basi tupeleke mpaka mara mbili, mara tatu, zipite, wananchi wafanye maamuzi ya kufanya biashara yao kwa urahisi zaidi. Hiyo nayo pia inaingia kwenye tija aliyoisema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, pia, kwa tukio ambalo limetokea kule Nyasa siku za karibuni, meli zetu ziliharibika kwa muda mrefu. Nayo pia inaweza kuwa siyo tija. Nataka niwahakikishie, tumeimarisha ukarabati wa hizi meli. Nimeenda Kyela, nimekuta meli zetu, tukaagiza wale watendaji wa *TASAC* waikamilishe kusimamia ukarabati wa zile meli na zianze mara moja. Taarifa ambayo tumezipata, meli zimeshaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, nayo pia inaleta tija katika utoaji huduma kwenye ukanda wetu. Kwa kufanya hilo tutaimarisha pia ukaguzi wa mara kwa mara, ili meli zisisimame wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunapunguza gharama za kuingia na kusafiri na kusafirisha mizigo ili kuvutia watu wengi

zaidi kutumia meli hizo. Nadhani huo ndiyo mkakati ambao tunaufanya ndani ya Serikali ili kuleta tija kwa Watanzania ambao tumekusudia kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Nyasa, pia tuna Mbunge hapa wa Kyela, tuna Mbunge hapa wa Ludewa, maeneo yote haya yananufaika na meli yetu kwenye Ukanda ule wa Ziwa Nyasa. Niwahakikishie Serikali itaendelea kutoa huduma kwenye maeneo hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Fatma Toufiq, uliza swali lako.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya usafirishaji hasa bodaboda imekuwa ni ajira kubwa sana kwa vijana, lakini kumekuwa kukitokea ajali ambazo zimekuwa zikisababisha vifo na ulemavu kwa vijana wetu kutokana na kukosa elimu ya usalama barabarani. Nini mkakati wa Serikali katika kutoa mafunzo ya mara kwa mara ili kuwaepusha nguvukazi hii na ajali hizi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Toufiq, Mbunge wa Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nami nikiri kwamba sekta ya bodaboda inayosimamiwa sana na vijana wetu imeweza kusaidia sana kupunguza tatizo la usafiri wa umbali mfupi mfupi na wakati mwingine hata umbali mrefu; na tunaona vijana wetu wa bodaboda wanafanya kazi nzuri. Pamoja na changamoto zilizopo, lakini huduma yao Serikali tunaitambua na tutaendelea kuisimamia ili iendelee kuboreshwa vijana

hawa waweze kufanya kazi hiyo kusafirisha watu, lakini wapate pato la mtu mmoja mmoja, linasaidia sana kwenye familia zao.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba zipo ajali zinazoweza kutokea au kwa bahati mbaya, lakini wakati mwingine kwa uzembe. Tunachofanya ni kuimarisha elimu. Jeshi letu la Polisi limekuwa na mpango mzuri kabisa wa kuwafuata vijana hawa kwenye maeneo yao na kutoa elimu. Watanzania tunaona baadhi ya makamanda wa Jeshi la Polisi wakiwa wako mbele za vijana wa bodaboda wanawaelimisha baadhi ya mambo ambayo wanatakiwa kuyazingatia ili wafanye kazi yao vizuri pamoja na kupunguza ajali pia.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana pia hata vyombo vya habari ambavyo vimekubali kutoa nafasi ya Jeshi la Polisi kwenda kutoa elimu kwa vijana wetu wa bodaboda. Tunaimarisha sasa kwa kila mwendesha pikipiki au bodaboda kwamba apate leseni na kuwahamasisha kuwa na angalau ile *helmet.* Yaani yale masharti yote yale ya usalama, kuendesha chombo cha moto waweze kuyakamilisha ili huduma hii iendelee kushamiri na iendelee kuwanufaisha wanaotumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali katika hili, nafasi yetu ni kuendelea kuimarisha utoaji elimu kwa vijana wanaoshughulika na bodaboda ili wajue kwanza kazi na thamani ya kazi yao. Pili wasaidie sana kwa kuzingatia sheria kupunguza ajali. Hili jambo ni muhimu sana na tumeendelea kulisimamia hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo la bodaboda kwanza Serikali tumelitambua na tumeendelea kuliimarisha na tutaboresha zaidi kwenye eneo hili. Pili mkakati huo wa kielimu tutaimarisha zaidi na tutawafikia wananchi, hao vijana wanaoshughulikia bodaboda mpaka kwenye vituo vyao ili kurahisisha na wao kuwaondoa kwenye maeneo hayo kwa

ajili ya kupata elimu. Kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha eneo hili na hayo ndiyo malengo ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, uliza swali lako.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Tarehe 10 Julai, Soko la Kariakoo liliungua, ambapo tarehe 11 Julai, wewe mwenyewe ulikwenda Kariakoo kwa ajili ya kuwapa pole wahanga na pia kutoa maelekezo ya Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunashukuru sana Serikali kwa sababu wamechukua jitihada za kujenga upya soko la Kariakoo ambako tarehe 6 Novemba, 2021 Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alikwenda Kariakoo kwa ajili ya kutoa maelekezo kuhusiana na kujenga Soko la Kariakoo, kulijenga upya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ramani mpya ya Soko la Kariakoo jipya ina masoko mawili ambapo kama sasa hivi yako masoko mawili. Ramani inataka na utaratibu wa kujenga unataka soko dogo na kubwa lijengwe kwa pamoja. Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili linaweza kupelekea ghasia na sintofahamu kwa wafanyabiashara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat, swali sasa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwa nini sasa Serikali isiweke utaratibu wa kujenga masoko haya kwa awamu ili wafanyabiashara wa soko dogo wabaki pale ili soko kubwa lijengwe halafu baadaye wahamishiwe likamilike kwa pamoja? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat, Mbunge wa Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulipata tatizo la soko la Kariakoo kuungua na wote tunajua, lakini Serikali imefanya jitihada kubwa sana. Tulienda kutembelea na kuwapa pole, lakini tulitaka tujiridhishe ajali ile ilitokana na nini? Tukaunda Timu ambayo pia ilifanya kazi yake vizuri na ikatupa mrejesho wa nini kilisababisha soko lile lakini Kamati ile ilienda mbali zaidi na kutuambia madhara ya soko lile yakoje.

Sasa lile soko pale lilipo limezungukwa na nyumba za watu binafsi, lakini pia kuna soko dogo liko karibu kabisa na lile soko, usalama wa soko lile dogo haukuwa mzuri pia nao. Kwa hiyo katika maoni au mapendekezo ambayo waliyatoa ile Tume ni pamoja na kuliondoa lenyewe na kulijenga lingine jipya ambalo pia litafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, atatutengea shilingi bilioni zisizopungua 32 mpaka 34 ambazo zitajenga masoko yote mawili na tumeona tufanye maboresho makubwa. Hawa walioondolewa kwenye eneo lile, kimsingi hata pale baada ya kuungua, hawa waliokuwa soko dogo walikuwa hawafanyi kazi zao. Nao tuliwasihi wapishe eneo lile, ili eneo lile sasa uchunguzi upite na sasa maandalizi ya ujenzi yaendelee na tumewapeleka Kisutu pamoja na eneo la *Machinga Complex* na wengine wameenda kwenye masoko jirani.

Mheshimiwa Spika, wale wote wameorodheshwa, wanafahamika nani alikuwa wapi. Malengo yetu, baada ya kukamilisha katika kipindi tulichokubaliana soko likamilike, wale wote waliokuwa soko dogo waliokuwa mle kwenye soko kubwa, tunawarudisha na kuwaweka kwenye nafasi zao. Kwa kuwa sasa soko tumeliboresha, soko dogo sasa tumelijenga kwenye ghorofa, ghorofa mbili mpaka tatu, tumeongeza na wengine waliokuwa wanazagaa kule nje wakakosa mahali, sasa tunawaingiza kwenye lile jengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote haya ni maboresho ambayo tumeyafanya ya kuhakikisha kwamba hawa walioko hapa si kwamba wanapata shida kubwa kwa sababu wengine

tumewapeleka pale Kisutu wanaendesha biashara zao na wale kwa sababu wana uhakika jengo likijengwa watarudi na watapata nafasi, naamini wanaiamini Serikali yao kwamba tutatenda hivyo na tutasimamia hilo ili kazi hiyo iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inasimamia kwa karibu na sasa iko kwenye zabuni ili ujenzi uanze katika kipindi kifupi, wafanyabiashara warudi kufanya biashara zao. Ahsanye sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, uliza swali lako.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kila mwaka Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya kupeleka kwenye Vyuo Vikuu ili watoto wasiokuwa na uwezo waweze kupata mkopo na kujikimu na mahitaji yao ya chuo. Utakubaliana na mimi kama Taifa tuna uhitaji mkubwa sana wa Watanzania hasa vijana wenye ujuzi hasa ujuzi wa kati ili sasa twende kuboresha na kupanua huduma muhimu kama vile afya, elimu, nishati na miundombinu vijijini. Sasa changamoto kubwa ya hawa vijana ambao tunawahitaji ambao wako kwenye vyuo vya kati hawana *access* ya hii mikopo na wao hawana uwezo wa kujilipia ada hizi.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha hawa vijana ambao tunawahitaji ambao wako kwenye vyuo vya kati wanakuwa na *access* ya kupata hii mikopo kama ambavyo tunafanya vijana wa elimu ya juu? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tweve, Mbunge wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Mbunge ni sahihi kwamba tuna kada ya elimu ya kati hawajaingia kwenye mkopo kama ambavyo mkopo huu unaendelea. Hii inatokana na sheria tuliyoiweka na ndiyo kwa sababu Bodi inaitwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Sheria iliyoanzisha Bodi hii ilianza kwa kuelekeza elimu ya juu na ndiyo ambayo sasa tunayo. Toka tulipoanza mpaka sasa tumegundua kwamba mahitaji ni mapana mno, lakini upana huu wa mahitaji utategemea pia na uwezo wa kifedha wa Serikali. Tukiwa tunaendelea kuwanufaisha Watanzania kupitia elimu ya juu kwa vyuo tu vya elimu ya juu, bado tuna mafanikio lakini tuna changamoto zake, tunaendelea nazo. Tumegundua tuna uhitaji pia wa elimu ya kati ambayo ni kada ambayo inafanya kazi kubwa sana kwenye sekta mbalimbali mpaka viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kadiri tunavyokwenda Serikali tutaleta Muswada ndani ya Bunge kama pia uwezo wa kifedha nao ukiwa mzuri na tutashiriki pamoja kujadili uwezekano wake ili kufungua mlango kwa vijana wa kada ya kati wa elimu ya kati ili na wao waweze kunufaika na mikopo hii. Kwa hiyo kadri tutakavyokuwa tunapata fedha, tutakuwa tunaendelea kuboresha kupanua wigo, tukifika elimu ya kati tutashuka mpaka elimu ya juu ya kawaida huku chini kwa maana ya sekondari kadiri tutavyopata fedha. Hiyo tutaileta Bungeni, tutajadili Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Tweve najua utakuwepo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Priscus Tarimo, uliza swali lako

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa hii nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sera ya kuwainua wananchi kiuchumi imekuwa na mafanikio sana kwenye ile mikopo inayotolewa na halmashauri kwa ajili ya akinamama, vijana na watu wenye ulemavu. Hata hivyo, kumekuwa na tatizo haswa kwa vijana, vijana wanavyopewa mikopo wakifikisha

umri wa miaka 35 vijana wa kike wanaenda kwenye kundi la akinamama, vijana wa kiume wanabaki hawana cha kufanya. Sasa swali langu, ni nini mpango wa Serikali wa kuwainua wanaume kiuchumi kwa sababu sera inasema ni wananchi kwa kufanya moja kati ya haya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wanaume makofi hayatoshi hayo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu kufuatia makofi hayo tunaomba majibu tafadhali, wanaume wote ukumbini hapa pamoja na wewe mwenyewe.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimo, Mbunge wa Manispaa ya Moshi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Mifuko kadhaa ambayo inawanufaisha Watanzania kulingana na eneo lile ambalo Mfuko huo umeanzishwa. Tunatambua kwamba kundi la vijana limechanganya maeneo yote, lengo pale ilikuwa ni vijana. Hata hivyo, iko Mifuko ya wananchi wote ambao pia wananufaika na Mifuko hii, lakini pia tumejiunganisha na taasisi za kifedha ambazo yeyote yule anakuwa na fursa ya kwenda kukopa.

Mheshimiwa Spika, tuliposema vijana, wanawake, wenye mahitaji maalum, Mheshimiwa Tarimo anajua kwamba sera ya nchi yetu sasa tumeelekeza katika kumwezesha mtoto wa kike, lakini na wanawake wote kwa ujumla ili na wao waweze kuchangia pato la nchi hii kwa kufanya shughuli mbalimbali. Kwa hiyo akishapata mkopo anaweza kuanzisha biashara na Mheshimiwa Tarimo anajua, ukimwezesha mwanamke unakuwa umeliinua Taifa hili. Ukimwelimisha mwanamke unakuwa umelielimisha Taifa hili. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuliona eneo hili, kwa kuwa tunatambua kwamba ukimwezesha mwanamke unaliwezesha Taifa hili, ukimwelimisha mwanamke

unaelimisha Taifa, kwa hiyo tuliona tuwawekee eneo lao ambalo wanakuwa na uhuru mkubwa wa kukopa. Anaweza kwenda kwenye Mfuko wa Halmashauri ambao una kipengele cha wanawake, anaweza kwenda Benki akakopa, anaweza kwenda kwenye Mfuko mwingine, Mifuko iko mingi, tuna Mifuko 42 ingawa sasa tutaipunguza ibaki michache, ifahamike kila mmoja aweze kwenda kukopa.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu bado hatujafikiria kuanzisha Mfuko wa Wanaume, lakini tayari wigo wa wanaume hao kupata mikopo upo kupitia Mifuko hiyo na taasisi za fedha. Hapo baadaye tukiona kuna umuhimu mkubwa, ama kuna udhaifu mkubwa pia tunaweza tukaanzisha kadiri itakavyowezekana. Sheria hizi na Mifuko hii tunapoianzisha tunaileta kwenye Kamati zetu za Bunge na kuona umuhimu wa kuanzisha hicho kitu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na mabadiliko ya tabianchi na ikolojia, kilimo cha umwagiliaji hakiwezi kukwepwa katika nchi hii. Miaka michache iliyopita Serikali ilitoa mabilioni ya fedha kununua vifaa vya uchimbaji wa mabwawa, lakini mpaka sasa hivi hakuna bwawa hata moja ambalo limechimbwa na hivyo vifaa vimechakaa na kwa sasa ni kama vile spana mkononi. Sasa nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba mabwawa haya yanachimbwa na kuwekeza fedha zaidi kwenye uchimbaji wa mabwawa ili kukinusuru kilimo chetu na mabadiliko ya tabianchi yanayoikabili nchi hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya kilimo, miaka yote nchini tumekuwa tukitegemea sana msimu wa mvua ili kuzalisha mazao yetu. Tumegundua kwamba tunayo fursa ya kutumia mabwawa yawe ya asili au ya kuchimba na kuyajaza maji tukatumia kwa kilimo cha kumwagilia. Tumeweka msisitizo kwenye eneo hili, pale ambapo tulichimba mabwawa mengi kwenye maeneo kadhaa lakini pia kuhakikisha kwamba tunakuwa na maeneo ya kumwagilia pale ambako kuna uwezekano mkubwa au kuna mvua nyingi na mabwawa yanajitengeneza. Serikali inaendelea kusimamia jambo hili kwa sababu tumegundua tukiimarisha kwenye umwagiliaji, tunafanikiwa sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali huko awali tulinunua mitambo hiyo ambayo Mheshimiwa Mwenisongole amesema imechakaa. Ni kweli, lakini kwa kuwa sasa tunakisimamia kilimo na maendeleo yake, Wizara ya Kilimo hapa hata walipokuja mbele yetu kuja kuomba kuongezewa bajeti, walieleza waliomba fedha ambayo Waheshimiwa Wabunge wameipitisha kwa ajili ya kuongeza mitambo mbalimbali kwa ajili ya kupanua wigo wa kilimo cha umwagiliaji. Lengo mitambo ile isambazwe kwenye kanda zetu na ifanye kazi ya kuchimba mabwawa kwenye maeneo hayo, yatumike kwa kilimo, lakini wakati mwingine pia na wafugaji watatumia kwa kunyweshea mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali ilishatoa fedha kwa ajili ya kununua mitambo hiyo ili kuendelea kuimarisha mitambo iliyopo kwa kununua vipuli ile iliyoharibika, lakini mipya kwa ajili ya kuendelea kuchimba mabwawa yetu. Kwa hiyo eneo hili tutaendelea kulisimamia kwa sababu tumegundua kwamba lina tija na hasa kipindi hiki ambacho tunaambiwa hali ya hewa ina badilikabadilika, kama tutakuwa na mabwawa na maeneo haya ya kumwagilia, tunaweza tukapata kilimo kizuri tu na tukavuna mazao mengi

tu kama ambavyo maeneo yote yenye mabwawa yanavyoweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mwenisongole kwamba, eneo hili kwa fedha ambayo tumeitoa, tutanunua mitambo na kama haitoshi tutaona uwezekano wa kuongeza ili iweze kufanya kazi ya kuchimba mabwawa katika maeneo yote kadiri ya uhitaji kwenye maeneo haya. Ahsante sana.

**SPIKA:** Swali la mwisho, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mradi wa kuchakata gesi unaofanywa katika eneo la Likong'o, Mkoani Lindi ni miongoni mwa miradi ya kimkakati ambayo imekusudia kuinua fursa za kiuchumi katika ukanda wa Kusini na Tanzania kwa ujumla. Nini maelezo ya Serikali kuhusiana na hatua iliyofikiwa ya mradi huu mpaka hivi sasa na Watanzania watarajie nini kutokana na mradi huu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna mradi huu mkubwa wa kimkakati wa *LNG* ambao uko Mkoani Lindi na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Kassinge anauliza swali na anayejibu ni mnufaika nambari moja. Mradi huu hatua tuliyofikia sasa ni nzuri, kwa sababu tayari *TPDC* wameshiriki kikamilifu kwenye hatua zote za awali ikiwemo na kulipa fidia wananchi wote waliokuwa kwenye eneo lile, wote wameshaondoka. Eneo lile sasa linaandaliwa kulima barabara mbalimbali huko ili

kuligawa kwenye *plots* zile ambazo huduma mbalimbali zitatolewa makazi, sehemu ya kuweka mitambo na maeneo ya utoaji wa huduma nyingine.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine muhimu zaidi ni ya majadiliano ambayo Wizara ya Nishati kupitia Waziri aliyepo sasa ameshaanzisha hiyo timu na wako Arusha kwa sasa wanaendelea ku-*negotiate,* kufanya majadiliano na yale makampuni. Makampuni yenyewe yako kama manne ambayo yameonesha nia ya kwenda kuwekeza pale eneo la Likong'o pale Mkoani Lindi kwa ajili ya kuchakata gesi.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ambao pia utaleta faida kwa Watanzania wote, tumeenda kuwahamasisha, nilikuwa ziarani Mkoani Lindi wiki mbili, tatu zilizopita. Nimetembelea eneo lile la huu mradi, nimekutana na wananchi na nimewaambia wananchi wajipange sasa kunufaika na huo mradi. Kutakuwa na mambo mengi, watakuja watu wengi, kutakuwa na shughuli nyingi, watu wajikite kwenye kilimo, walime mazao yatakayoweza kuuza, watu wafuge watauza, lakini na huduma nyingine hoteli na nyumba za kulala wageni, ziandaliwe. Hizo ndiyo fursa ambazo tunazipata kwa kuwa na miradi mikubwa ya kimkakati kama wa *LNG*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Watanzania wategemee mafanikio makubwa kwa mradi huu ambao tayari mchakato wake unaenda katika hatua nzuri ya kwenda kuanza uchimbaji, uanzaji wa kuchimba na kuwekeza kwenye mradi huo. Kwa hiyo kwa ujumla wake miongoni mwa miradi mikubwa nchini ambayo pia ni ya kimkakati umo na mradi huu ambao utatengeneza fursa nyingi ikiwemo na ajira kwa Watanzania wote, kwa Watanzania wale ambao watapata nafasi ya kuajiriwa kwenye eneo lile. Hizo ndiyo fursa ambazo zinatarajiwa na Watanzania kupatikana kupitia mradi huo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwa kujibu maswali yetu. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, matarajio yetu ni kwamba Serikali pamoja na majibu

mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametupatia, itaenda kuangaliaangalia hali ya wanaume, kuona namna gani, namna gani. Ahsante sana Mheshimiwa *Prime Minister.*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Maswali ya kawaida.

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya kawaida, tunaanza na Mheshimiwa Latifa Hamis Juakali, Mbunge wa Viti Maalum, Zanzibar akiuliza swali lake kuelekea Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Latifa tafadhali.

Na. 79

**Vijana Kuhamasishwa Kushiriki Katika Shughuli za Uzalishaji mali**

**MHE. JUDITH S. KAPINGA K.n.y. MHE. LATIFA K. JUAKALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwahamasisha Vijana kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali?

**SPIKA:** Majibu, Ofisi ya Waziri Mkuu, nani? O*k,* nimekuona, tafadhali endelea na majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juakali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mikakati mbalimbali ya kuboresha mazingira yatakayoleta tija kwa

vijana na kuwahamasisha kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Mikakati hiyo ni pamoja na ifuatayo:-

(i) Kutoa mikopo yenye riba nafuu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya vijana, ambapo hadi kufikia Oktoba, 2021 jumla ya vikundi vya vijana 957 vimewezeshwa kupata mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 6.7 ambayo imechochea ufanyaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi;

(ii) Kutoa mikopo isiyo na riba kupitia asilimia nne ya mapato ya ndani ya Halmashauri, ambapo hadi kufikia Juni, 2021 zaidi ya vikundi vya vijana 15,349 vimewezeshwa kupata mikopo yenye thamani ya Shillingi Bilioni 54.7;

(iii) Tumeendelea kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali, ambapo hadi sasa Halmashauri 111 zimetenga maeneo yenye ukubwa wa ekari 217,802 ambayo yamewanufaisha vijana 3,232; na

(iv) Tunaendelea kuendesha programu za mafunzo katika fani mbalimbali ikiwemo za ukuzaji ujuzi, Uanagenzi, Urasimishaji ujuzi pamoja na mafunzo ya kilimo cha kisasa. Kupitia mafunzo hayo, vijana 43,881 wamepatiwa mafunzo ya uanagenzi, Vijana 20,334 wamepata mafunzo ya kurasimisha ujuzi na Vijana 12,580 wamewezeshwa kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa kupitia teknolojia ya kitalu nyumba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mikakati hii vijana wameweza kujipatia ajira pamoja na kujikita kwenye miradi ya uzalishaji mali ambayo imeendelea kuchangia ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri Ummy Nderiananga, nimekuona Mheshimiwa Judith.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya

Serikali naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya maeneo yanayoweza kuongeza ajira kwa vijana ni eneo la kuongeza thamani kwenye bidhaa. Je, Serikali inamkakati gani wa kuja na programu zinazoweza kuwasaidia vikundi vya vijana vinavyopata mikopo ya halmashauri kuweza kuongeza thamani kwenye bidhaa ambazo inazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; ni kutokana na mabadiliko mbalimbali ikiwemo ya Sayansi na Teknolojia zipo ajira mbalimbali zinazoweza kuzalishwa kutokana na mabadiliko hayo. Je, Serikali inamkakati gani wa kufanya maboresho ya sera ya vijana ili vijana waweze kupata ajira kutokana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea hususani katika Sekta ya Sayansi na Teknolojia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwanza kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Judith Kapinga amekuwa akifanya kazi kubwa ya kutushauri Serikali katika eneo hili hongera sana Mheshimiwa Judith. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la kwanza anauliza kuhusu kuongeza thamani, Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan tunaendelea kuhakikisha kwamba tunawaunganisha vijana na fursa hizi mbalimbali tunashirikiana na wenzetu wa *SIDO* na *UNIDO* tuna mfano hai wa vijana wetu wa Kampuni ya JATU wanafanya vizuri kuongeza thamani, mazao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna vijana wa Kiwanda cha Chaki kule Maswa, tuna vijana pia wa Kiwanda cha Mabegi Mwanza na vijana wengine na tunaendelea bado kuhakikisha kwamba vijana wetu wanaongeza thamani vitu

wanavyozalisha badala ya kuuza *raw material* na tutaendelea kuendelea kutilia mkazo katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, anataka kufahamu ni lini tutaleta sera hii; tupo katika hatua nzuri na tayari kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tumeshakusanya maoni kwa wadau wote wanaohusika na masuala ya vijana na tumemaliza sasa tuna rasimu ya kwanza ambayo inafuata utaratibu wa kiserikali na baadaye tutaendelea kuwafahamisha kwamba tumefika hatua gani, lakini tunaweza kuahidi tu kwamba kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa fedha tutakuwa tayari tuna sera ya vijana. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata bado tunaelekea Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali litaulizwa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya Mbunge wa Nyasa, tafadhali.

Na. 80

**Kuongeza Mtandao wa Barabara-Mbamba Bay**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa kipaumbele wa kuongeza mtandao wa barabara za lami za Mji Mkongwe na wakitalii wa Mbamba Bay?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya Mbunge wa Jimbo la Nyasa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini *(TARURA)* inaendelea na ujenzi wa lami kilometa moja unaogharimu jumla ya shilingi milioni 473.50 unaotekelezwa na Mkandarasi *VAG Contractors Ltd.* katika eneo la Makao Makuu ya Wilaya kwa maana ya Bomani kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na ujenzi wa kilometa 0.5 Kata ya Kilosa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa eneo la Mbamba Bay kama eneo la utalii na shughuli za Uvuvi. Hivyo, Serikali itaendelea kutenga fedha kujenga barabara kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha katika eneo la Mbamba Bay.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Stella nimekuona umesimama au bado. Uliza swali lako Mheshimiwa *Engineer* Stella*. (Makofi/Kicheko)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kuishukuru sana Serikali kwa jitihada kubwa ambazo zimeshaanza katika kuboresha Mji huu wa Mbamba Bay. Lakini pamoja na shukrani hizo, ninapenda kupata majibu kutoka Serikalini, Mji huu wa Mbamba Bay ni mji ambao ni wa muda mrefu sana takribani miaka mia moja, lakini vilevile ni kitovu cha utalii katika Mkoa wa Ruvuma, lakini hiki kiasi cha kilometa moja, moja na nusu kinachotengwa ni kidogo kulinganisha na mahitaji yaliyopo kwa sababu mji huu umedumaa kwa muda mrefu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba katika bajeti inayofuata angalau tupate hata kilometa mbili ili kuendana na kasi ya kukuza utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Jimbo la Nyasa ni kubwa sana kwa ukubwa wake na jiografia milima mikali kiasi kwamba hawa *TARURA* ambao wanasimamia hizi barabara wanapata shida sana katika usimamizi kutokana na kuwa na gari bovu ambalo kila wakati linaendea matengenezo kutokana na hali halisi ya mazingira.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza gari jipya moja angalau kuwawezesha hawa watumishi wa *TARURA* waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Silinde Naibu Waziri TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya Mbunge wa Jimbo la Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mji wa Mbamba Bay ni Mji mkongwe na Mheshimiwa Mbunge kama alivyozungumza nafahamu jitihada kubwa ambazo anazifanya katika Jimbo lake na anahitaji tuongeze bajeti kuhakikisha ule mji unaongezewa lami.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza katika swali letu la msingi kwamba tutaendelea kutenga fedha na katika mwaka wa fedha unaokuja kwa maana ya 2022/2023 basi Mji wa Mbamba Bay tutauongezea bajeti kwa ajili ya ujenzi wa kilometa walau moja ya lami nyingine ili kuongeza mtandao wa lami katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili ameeleza kwamba Halmashauri ya Nyasa gari lake watu wa *TARURA* ni bovu na wanashindwa kufika katika maeneo korofi ni muhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini tumeshaagiza magari mia moja ambayo tutayagawa katika Halmashauri za Wilaya 100 nchini ikiwemo Halmashauri ya Nyasa.

Kwa hiyo, hilo tunauhakika nalo atapata gari jipy. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea Mheshimiwa Tabasam.

Na. 81

**Kuzipandisha Hadhi Shule za Sekondari kuwa na Kidato cha Tano na Sita -Sengerema**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza:-

Je, mpango wa kuzipandisha hadhi Sekondari za Ngweli, Ngoma A, Tamabu, Nyamatongo, Sima, Nyampande na Katunguru kuwa za Kidato cha Tano na Sita Wilayani Sengerema umefikia wapi?

**SPIKA:** Bado tupo TAMISEMI bado tupo kwako Mheshimiwa Silinde majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao Mbunge wa Jimbo la Sengerema, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa spika, kabla ya shule kusajiliwa Kidato cha Tano na Sita inatakiwa kuwa na miundombinu ya msingi kwa ajili ya kupokea wanafunzi. Jukumu la ujenzi wa miundombinu hiyo si la Serikali kuu tu bali ni la halmashauri kupitia mapato yake ya ndani pamoja na wadau wa elimu na jamii nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Mkurugenzi wa Halmashuri ya Wilaya Sengerema na kuwasiliana na Ofisi ya Uthibiti Ubora kufanya tathmini katika Shule za Sekondari za Ngweli, Ngoma A, Tamabu, Nyamatongo, Sima, Nyampande na Katunguru ili kujiridhisha na hali ya miundombinu ya msingi kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga miundombinu katika baadhi ya shule zilizopendekezwa

kuanzisha Kidato cha Tano na Sita kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha ili kuongeza fursa ya Elimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam nimekuona.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sengerema tunazo shule 31 za Sekondari na katika hizo shule 31 Sekondari mbili ndiyo zina kidato cha Tano na Sita, Sengerema Sekondari na Nyampurukano Sekondari na zimeelemewa wanafunzi na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja aliona ile hali ya Sengerema kwa watoto walivyowengi na wananchi wa Sengerema wanamshukuru Mwenyezi Mungu wanaendelea kufanya kazi ya ziada kwa ajili ya kuwashughulikia akinamama kupata watoto wengi kuijaza dunia.

Mheshimiwa Spika, sasa hili jambo la Sengerema kutokukosa Sekondari hizi za Kidato cha Tano, Sengerema wanafunzi wanakosa nafasi na Mheshimiwa Naibu Waziri aliona na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alikuja kule na akaona hiyo hali. Lini sasa hili jambo litafanyika kwa haraka kwa ajili ya huyo Mdhibiti Ubora kwenda kukagua hizi shule kwa sababu zimekaguliwa mwaka huu na mwaka kesho tunategemea wanafunzi watakuwa ni wengi nini msaada wa wizara katika jambo hili, la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili ni kwamba Sengerema Sekondari imeelemewa na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alikuja pale na akatoa ahadi ya kutupa vitanda kutokana na watoto alivyoona wanalala katika mazingira magumu na Nyampurukano Sekondari pia imeelemewa ni nini msaada wa Serikali katika jambo hili ili waweze kutusaidia kwa haraka sasa katika kuzisajili shule hizi.

**SPIKA:** Ahsante sana maswali yako yameeleweka kwa kuwa hamlali sasa sijui Mheshimiwa Waziri afanye nini. Mheshimiwa Silinde. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika,

naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamis Tabasamu Mbunge wa Jimbo la Sengerema niweze kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ameeleza kwamba katika halmashauri yake ya Sengerema kuna Sekondari karibu 31 na katika hilo eneo kuna shule mbili tu za kidato cha tano sita na anataka kwamba tuwaagize watu wa Udhibiti Ubora kwamba waende wakakague hizi shule tuone kama zinakidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, na ni nitumie fursa hii najua kwamba kazi nzuri ambayo anaifanya Mheshimiwa Mbunge na bahati nzuri nilifika pale na niliona jitihada yake kubwa kujenga shule 15 kwa mpigo. Niwaagize tu Halmashauri ya Sengerema kwamba waende sasa hivi huko walipo kuanzia wiki ijao wakague na watuletee taarifa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kama maeneo haya yanakidhi vigezo ya kuanzishwa kidato cha tano na cha sita na kwa sababu tunaile programu yetu ya kuzipanua shule 100 kwa ajili ya kuziongezea madarasa na miundombinu ili kuzifanya kuwa kidato cha tano na cha sita. Kwa hiyo, tutazingatia katika ule mpango ili tuone tunaweza tutaongeza shule ngapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kwamba Mheshimiwa Waziri alifika kule na aliahidi nimwambie tu kabisa kwamba najua alifika shule eneo la Sengerema na aliahidi kutoa baadhi ya vitanda kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi ya wanafunzi ama waweze kupata malazi bora. Kwa hiyo, ahadi ile ipo pale pale na itatekelezeka kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alikuwa ameahidi na nikuhakikishie tu kwamba shule zote ambazo zitakidhi vigezo basi tutaziingiza katika mpango. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasamu haina uhusiano wa moja kwa moja kwa watoto kwa Watoto wa kidato cha tano na sita wanasambazwa na Waziri wa Elimu nchi nzima. Kwa hiyo, haina maana kwamba mkijenga shule nyingi za *A-level* pale, zitatatua tatizo la Sengerema peke yake, inasaidia

matatizo ya nchi kwa jumla wake. Kule Msekwa nimemuona Mheshimiwa Venant Protas.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto la Jimbo la Sengerema ni sawa sawa na Jimbo la Igalula.

**SPIKA:** Ongeza sauti, ongeza sauti.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igalula hatuna shule ya kidato cha tano na sita, lakini baada ya kutambua hayo wadau na wanachi tumeweza kujikongoja na tumepata mabweni na miundombinu salama ya kuweza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Je, lini Serikali itaitambua shule ya Sekondari ya Tula ili iweze kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita ili kupunguza uhaba wa shule katika nchi hii?

**SPIKA:** Ahsante sana pale Tula kuwe na kidato cha tano na sita, majibu Mheshimiwa Silinde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Venant Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba katika maeneo yale ambayo yanahitajika kuanzishwa kidato cha tano na cha sita ni lazima halmashauri husika kupitia Ofisi za Elimu pamoja na watu wa Udhibiti Ubora wanakwenda katika eneo husika wanakagua ile shule, wanatuletea hayo mapendekezo tunaona kama ina *meet* vile vigezo.

Kwa hiyo, kama inafikisha vile vigezo basi sisi tutakuwa tayari kuongeza fedha na baadhi ya miundombinu ili kuhakikisha tunaisajili na kupokea. Kwa hiyo, na yeye Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tutawaagiza watu katika halmashauri yake watatuletea hiyo taarifa na baada ya hiyo

taarifa maana yake tutaleta majibu ya msingi kama inakidhi kupandishwa au itasubiri katika mwaka mwingine wa fedha. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Monni nilikuona Mbunge wa Chemba.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, shule ya Sekondari Farukwa ilipandishwa hadhi na ikawa ya kidato cha tano na sita lakini baadaye wakasitisha na sababu walizofanya wasitishe tumezimaliza tayari ni lini sasa watarudishia shule yetu ya kidato cha tano na sita. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya shule ya Farukwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Monni Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anasema kwamba Shule ya Farukwa ambayo ipo katika Jimbo la Chemba wameshamaliza zile changamoto kwa hiyo wanataka kujua ni lini sasa Serikali itairudisha ile shule ili sasa ianze kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tutawatuma wataalam kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI watakuja kukagua kujiridhisha kama hizo vile vigezo vyote mmeshamaliza na kama itakuwa imekamilika basi nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mwaka unaokuja hiyo shule itafunguliwa na wanafunzi wataenda kusoma hapo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga nilikuona.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante Jimbo la Makete linakata 23, kata tatu hatuna shule za Sekondari na katika vipaumbele ambavyo nilivileta kwenye wizara ni Kata ya Mlondwe ndiyo ianze kujengwa shule ya

Makete *Boys* na tuliahidiwa kupewa milioni mia 600, lakini hadi sasa milioni 600 hatujazipata.

Je, ni lini milioni 600 zitafika ili tuanze ujenzi wa Makete *boys* na baadaye tufuate shule Kigala na baadaye tufuate shule ya sekondari Bulongwa? Naomba majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI tunakuomba majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde kwa majibu mazuri sana kwa maswali yaliyotangulia nimesimama kuhusu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Sanga ni lini shilingi milion 600 zitatoka kwa ajili ya kujenga sekondari katika Kata ambazo hazina sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekamilisha orodha ya sekondari 214 za kila Jimbo ambazo zitapata shilingi milioni 600, lakini Mheshimiwa Dkt. Mwigulu amesema atatupa shilingi milioni 470 kilichonikwamisha hatujatoa mkeka Waheshimiwa Wabunge wanabadilisha mara kwa mara. Kwa hiyo, hapa simu yangu imekufa nilikuwa nitoe taarifa na ndiyo maana nimesimama kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kujiridhisha na kile kipaumbele ulichoweka cha Kata yako nitatuma ujumbe kwenye *group* la Wabunge kusema umpigie mtu gani, uangalie je, hiyo kata yako iliyowekwa ndiyo kata ya kipaumbele. Lakini Mheshimiwa Dkt. Mwigulu yuko tayari tumekwama sisi kwa sababu Wabunge wanabadilisha badilisha.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ile shule ya Mkoa mmoja na waomba sana Waheshimiwa Wabunge tuliomba mchakato uanze kwenye *RCC*. Kwa hiyo, tumeandikiwa barua na Makatibu Tawala wa Mikoa, wakisema kwamba shule ile moja. Kwa hiyo, kutakuwa na 214 za kila Jimbo, halafu tutanza na moja ya kila mkoa, naomba sana Wabunge mapendekezo yametoka kwa Makatibu Tawala wa Mikoa. Kwa hiyo, tunaomba sana tumeona kuna watu

wanabadilisha toa wilaya hii peleka hii sisi tumezingatia ushauri wa Makatibu Tawala wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, *by* tarehe 15 Mheshimiwa Sanga mkitupa *confirmation*, hela Mheshimiwa Dkt. Mwigulu yupo tayari zitakuwa zimeshaenda kwenye halmashauri zenu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa mnapiga makofi lakini jamani vitu vingine kidogo vinataka... wanaenda kupewa milioni 600, milioni 600 wale ambao Kata ambazo hazina Sekondari ukilitizama *superficially* ni jambo jema. Lakini una m-*reward* mtu ambaye alikuwa hajishuhulishi na chochote yule ambaye ana madarasa manne, matano, sita alijitahidi, lakini bado hana madarasa ya kutosha yeye anaachwa wakati hao wamejitahidi, wamejitahidi huyu anapata mia 600 hawajafanya chochote wamelala tu na hawana sekondari, kidogo sera za namna hii tuwe tunaziangalia jamani. Kwa sababu, anayefanya juhudi ndiye anaachwa yule ambaye hafanyi juhudi yoyote anapata 600 *hundred million. (Makofi/ Kicheko)*

Serikali tunaomba muwe mnaangalia sisi tunaishi sana vijijini tunajua kwamba Mbunge anaishi vijijini anajua hata wale wanaofanya juhudi wanachukia wanaona wale ambao hawaangaiki chochote wanapata milioni 600, wao ambao wamejiangaisha wana madarasa manne, matano wameanza *form one* wanataka waingie *form two* wao hawana chochote.

Kwa hiyo, ni yakuliangalia vizuri hili jambo tusiwavunje moyo wananchi wetu hawa wasio na chochote nao wapate na hawa waliofanya juhudi kidogo nao wapate, hiyo itakuwa ni jambo jema. *(Makofi)*

Wizara ya Mifugo na uvuvi Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo wa Kibaha Vijijini. Maana kwa nini ninyi msiwe na sekondari mpaka leo kwenye Kata zenu, kwa nini wamelala hao na unaweza ukakuta hata choo hawajachimba hiyo Kata. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Ulega aah! Mheshimiwa Mwakamo kwanza uliza swali lako.

Na. 82

**Ranchi za Taifa Kutumiwa na Wafugaji**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza: -

Je, ni Ranchi ngapi nchini zimeshawapokea wafugaji na kuwapatia nafasi ya kufuga kwenye Ranchi hizo kama Serikali ilivyotoa maelekezo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo Mbunge wa Kibaha Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* imetekeleza maelekezo ya Serikali kwa kutenga jumla ya vitalu vya muda mrefu 116 katika Ranchi 11 za *NARCO* na kuzikodisha kwa wafugaji wadogo 116. Ranchi hizo ni Kikulula (Kagera) vitalu 2, Mabale (Kagera) vitalu 7, Kagoma (Kagera) vitalu 18, Kitengule (Kagera) vitalu 10, Missenyi (Kagera) vitalu 11, Mkata (Morogoro) vitalu 7, Dakawa (Morogoro) vitalu 2, Mzeri Hill (Tanga) vitalu 9, Usangu (Mbeya) vitalu 16, Kalambo (Rukwa) vitalu 13 na Uvinza (Kigoma) vitalu 21. Jumla ya eneo la vitalu hivi ni hekta 322,525.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kutatua migogoro ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini hasa baada ya wafugaji kuondolewa kwenye hifadhi za misitu na mapori ya akiba, Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* ilianzisha utaratibu wa kugawa vitalu vya muda mfupi ambapo jumla ya vitalu 128 vimekodishwa kwa wafugaji wadogo 128 kutoka katika Ranchi 10 za *NARCO*. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenye majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri hajaeleza na wala hajaitaja Ranchi ya Ruvu iliyopo pale Vigwaza kama imeshatengwa, sasa kwa kuwa kuna migogoro mingi ya wakulima na wafugaji kwenye Mikoa ya Pwani na maeneo mengine ya jirani kama Wilaya ya Chalinze na Kibaha Vijijini; Je, Serikali haioni huu ni muda sahihi sasa kupanga na Ranchi ile ili kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji kwenye maeneo hayo?

Swali la pili; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba migogoro mingi ya wakulima na wafugaji inapelekea watu wengi kupata ulemavu wa kudumu na wengine kufariki na kwa sababu ipo Ranchi hiyo ninayoitaja ya Ruvu ambayo haijafanyiwa; Je, Waziri haoni kwamba ni muda sahihi wa kufika kwenye maeneo ya Mkoa Pwani hasa Wilaya hizo za karibu kuwaelimisha wafugaji wadogo kwenda kuomba na kupata utaratibu wa kukaa kwenye Ranchi hizo kuondoka kwenye Bonde la Ruvu ambalo lina migogoro? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ulega majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru na kumpongeza sana lakini pili kwanini Ranchi ya Ruvu haikutamkwa katika majibu haya. Ranchi ya Ruvu katika maelekezo ya muda mrefu uliopita ya Serikali haikupangwa kwa ajili ya vitalu vya muda mrefu. Ranchi ya Ruvu na Ranchi

ya Kongwa hazikupangwa. Kwa hivyo, baadaye kwa utashi na maelekezo ya viongozi wetu wakuu na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutaka kuona tunatatua changamoto ndiyo uamuzi wa kukata vitalu vya muda mfupi ukafanywa kwa hivyo Ranchi ya Ruvu ikapangiwa ikatwe vitalu jumla ya 19 na hivi sasa ninavyozungumza jumla ya Ng'ombe zaidi ya Elfu Tisa katika vitalu hivi vidogo vidogo vilivyopo katika eneo nzima la Ranchi Ruvu vimeshagawiwa kwa wafugaji, hili ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni namna ya kuweza kuwatoa wale wafugaji walioko katika maeneo ya Bonde la Mto Ruvu na labda kuwapa nafasi huku. Serikali jambo hili inalifanyia kazi siyo peke yake katika Mto Ruvu lakini vilevile na mito mingine kama Kilombelo, Ruaha na mingineyo. Maelekezo ya Serikali ni kwamba iko Kamati ya Mawaziri Nane inayofanya tathmini ili tutakapotoka na majawabu, tutatoka na majawabu ya pamoja yatakayokwenda kutatua kabisa tatizo hili la muda mrefu la wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete nilikuona uliza swali la nyongeza.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, nami naomba niulize swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya jumla ya hekta 2,208 zimegawiwa kutoka kwenye Ranchi ya Ruvu kwenda kwa wanavijiji vinavyozunguka au katika Halmashauri ya Chalinze vikiwemo vijiji vya Kindogonzelo, Kitonga, Magulumatali, Vigwaza na Milo. Je, ni lini Serikali inakuja kutukabidhi vipande hivyo vya ardhi kwa ajili ya wananchi wetu sasa kuweza kugawana ili kuweza kutengeneza utaratibu mzuri wa kufuga. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Inaelekea Wazaramo walitokana na Wagogo, majina mengi ya kigongo kigongo Magulumatali maana yake ni miguu mirefu, Majimatitu, maana yake maji meusi,

Mabwepande maana yake ni mawe, mabwe ni mawe. Mheshimiwa Ulega majibu.*(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana umetupa elimu nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali zuri la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Chalinze Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba tumetenga hekta 2,208 hii ni kwa sababu ya lile jibu la msingi nililolitoa lililoulizwa na Mheshimiwa Mwakamo la kuondosha migogoro kati ya wakulima na wafugaji ni moja ya jitihada za Serikali na utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, tayari hatua za mwanzo za kiutawala ndani ya Wizara zimeshafanywa, vimeshapimwa na kutengwa maeneo haya, hatua inayofuata sasa ni kwenda kuwakabidhi Halmashauri ya Chalinze na Kibaha na hasa Jimbo la Chalinze, Jimbo la Kibaha Vijijini na Jimbo la Bagamoyo. Mara tu baada ya Bunge Wizara itakuwa iko tayari kabisa kuhakikisha kwamba sherehe hizi za kwenda kuwakabidhi na waweze kujipangia matumizi zinakwenda kufanyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tuendelee tu, naona na wengine katika Ukumbi wa Msekwa tu kule lakini tuendelee. Swali la Mheshimiwa Mohammed Soud Jumah, Mbunge wa Donge.

Na. 83

**Wizi wa Mazao ya Kilimo na Mifugo Zanzibar**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani ya kupunguza au kuondosha kabisa wizi wa mazao ya kilimo na mifugo katika maeneo ya Unguja na Pemba.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi nimekuona Mheshimia Hamza Khamis Khamis.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi nchini ndilo lenye jukumu la kulinda maisha na mali za wananchi na linatambua suala la uhalifu na wizi wa mifugo na wizi wa mazao ya kilimo unaosumbua wananchi wa Zanzibar, katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Septemba 2021 jumla ya matukio 72 ya wizi wa mifugo na 85 ya wizi wa mazao umeripotiwa katika vituo vya Polisi. Watuhumiwa 48 wa wizi wa mifugo na 52 wa wizi mazao wamekamatwa na kesi 22 za wizi wa mifugo na 36 za wizi wa mazao zinaendelea mahakamani na ziko kwenye hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi kuanzisha na kushiriki kwenye vikundi vya ulinzi shirikishi ili kuzuia uhalifu na Jeshi la Polisi litaendelea kufanya doria kwenye maeneo yote ili kudhibiti na kutokomeza uhalifu hapa nchini. Nakushukuru.

**SPIKA:** Hivi mtu akiiba mifugo Zanzibar kule anapeleka wapi? Mheshimiwa Mbunge wa Donge uliza swali lako. *(Kicheko)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wizi wa mazao ya kilimo na mifugo yamekuwa yakiongezeka pamoja na takwimu nzuri ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezieleza hapa.

Je, ningependa Mheshimiwa Naibu Waziri alieleze Bunge lako Tukufu tuna-*fail* wapi?

Swali Namba Mbili, ningeomba vilevile kuuliza kwa sababu kinga ni bora kuliko tiba. Je, hatuoni kwamba kuna haja ya kukinga haya matokeo ya wizi yasitokee ili kuwasaidia wananchi na wakulima wasiweze kupata hasara ya kuibiwa mazao yao. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge mimi nina wasiwasi wale Wanyamwezi wale ndiyo wanaoiba mifugo kule, Mheshimiwa Waziri anashindwa kuwataja tu hapa. Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani anauliza mna-fail wapi na hawa Wanyamwezi? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Soud Mbunge wa wananchi wa Jimbo la Donge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi wajibu wetu mkubwa ni kulinda raia na mali zao. Kwa hiyo katika hili tunajitahidi na tunafika hatua tunakuwa tunakutana na changamoto nyingi zikiwemo zile za wananchi wenyewe kwanza kushindwa kwenda kutoa ushahidi kwamba nani ameiba na nani amechukua mazao na nani amechukua mifugo. Lakini kikubwa ni kwamba tunaendeleza jitihada za kuhakikisha kwamba tunawakamata tunawafikisha kunako vyombo vya sheria hawa wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali katika kuzuia haya, tuna mikakati mingi ambayo kama atarejea kwenye jibu langu la msingi moja ni kuendeleza ule ushirikishwaji wa wananchi katika ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ambalo pia tumelifanya kama ni sehemu ya mkakati ni kufanya doria za mara kwa mara katika maeneo haya hasa yale maeneo ya Zanzibar maeneo ya Donge, Muwanda na maeneo mengine ili lengo na madhumuni hivi vituko ama hivi vitendo vya uhalifu

visiweze kutokea. Lakini kubwa nataka nitoe wito kwa wananchi wetu wasiendelee kuchukua hatua mikononi mwao, tumepata matukio mengi ya watu wanachinjwa, watu wanachomwa, watu wanachukuliwa hatua mikononi kitu ambacho ni kinyume na utaratibu wa sheria. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kule Msekwa nimekuona Mheshimiwa Neema Mwandabila uliza swali lako.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali...

**SPIKA:** Ongeza sauti.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsate kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Momba ina Halmashauri mbili. Halmashauri ya Mji wa Tunduma na Halmashauri ya Wilaya Momba. Makao Makuu yapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba sehemu ambayo ni mbali kutoka Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Katika hali ya usalama Tunduma ina hali hatarishi zaidi kuliko Wilaya ya Momba nilitamani kufahamu ni lini Serikali itaweka Wilaya mbili za kipolisi katika Wilaya ya Momba yaani Mji wa Tunduma pamoja na Halmashauri ya Momba. Ahsante.

**SPIKA:** Nafikiri lengo lake pia kupunguza wizi wa mifugo na mazao. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kwa kifupi sana swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mwandabila kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, suala la uwekaji wa Vituo vya Polisi au uwekaji wa huduma hizi za ulinzi na usalama zinategemea mambo mengi sana, ukiwemo utaratibu wa kuangalia kwanza mahitaji ya eneo hilo, kwa sababu inawezekana kuna

mahali vituo vipo karibu na huduma zipo karibu, lakini kikubwa ni kwamba nimwambie tutakwenda tukakague ili tuone kama tutaona kuna haja ya kufanya hivyo basi tutaweka. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado tupo kwako Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Nusrat Shaban Hanje uliza swali lako.

Na. 84

**Kutenganisha Mahabusu/Magereza ya Watoto na Watu Wazima**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza: -

Je, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kutenganisha Mahabusu/Magereza ya Watoto na Watu wazima ili kuwalinda Watoto dhidi ya vitendo vya ukatili wa kingono vinavyoweza kujitokeza.

**SPIKA:** Haya majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kutoka kwa wazoefu wa huko. *(Makofi/ Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifutavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kulinda haki ya mtoto, Serikali ilitunga Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 ambayo inakataza kifungo kwa watoto na kuweka mahabusu magerezani na iwapo italazimu kuwekwa mahabusu sharti awe chini ya uangalizi wa Kamishna wa Ustawi wa Jamii au mahabusu za nyumbani au chini ya uangalizi wa taasisi yeyote itakayotamkwa katika amri ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Jeshi la Magereza za Mwaka 2003 Toleo la 4, chini ya Kanuni 488 zimeweka utaratibu mzuri wa kuwatenga wafungwa na mahabusu katika sehemu maalum na vyumba maalum kwa kuzingatia umri ambapo wafungwa na mahabusu watoto hutengwa katika mabweni yao maalum pasipo kuchanganywa na wakubwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali inalo Gereza la Wami ambalo ni maalum kwa watoto ama vijana waliokatika ukinzani wa sheria na kuhukumiwa vifungo ambavyo huhamishiwa huko na kutumikia vifungo vyao wakiwa peke yao kama vijana bila ya kufungwa na watu wazima.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali inaendelea kuwalinda watoto dhidi ya ukatili wa kingono na ukatili mwingine na kusimamia ipasavyo Sheria ya Watoto na Sheria zingine nchini zinazotoa ulinzi kwa watoto. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nitauliza maswali pamoja na majibu hayo...

**SPIKA:** Mnao simama maswali ya nyongeza muwe na uzoefu siyo mnataka tu kutupotezea muda hapa, Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nitauliza maswali mawili ya nyongeza kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba amezungumiza suala la Kanuni za Magereza ambazo zinataka watoto watengwe tofauti na watu wazima wanapokuwepo Mahabusu. Mlundikano wa Mahabusu kwenye magereza zetu hauruhusu jambo hilo ni kwa nini sasa Serikali isiongeze au isipeleke Maafisa Ustawi wa Jamii ambao watakuwa wanashughulika na Watoto wanapokuwa kule kwa sababu ni vigumu sana ku-*monitor.* Kwa mfano, Gereza la Segerea

kuna mahabusu si chini ya mia moja watoto na Maafisa wapo wawili tu ME na KE. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili; kwa nini sasa Serikali isipitie upya kujua idadi ya watoto ambao wana kesi kwenye Mahakama zetu na kwenye Mahabusu zetu yaani kwa maana ya Magereza ili sasa ile sheria kwa jinsi ilivyowekwa na ni nzuri, lakini utekelezaji wake ni mgumu ni kwa nini sasa wasipitie upya ili kuhakikisha kwamba watoto hawa wanasaidiwa kwa sababu hali za watoto wetu kwenye Magereza zetu ni mbaya mno. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje Mbunge wa Viti Maalum, nayo nayajibu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa atarejea kwenye jibu langu la msingi atagundua kwamba kuna sehemu nimesema kutakuwa kuna Maafisa wa Ustawi ambao watakuwepo maalum katika magereza kwa ajili ya kusimamia haki na maslahi na kuwalinda watoto hawa. Kwa hiyo, kama changamoto ni Maafisa hawa kuwa kidogo basi nimhakikishie tutajitahidi Serikali kupitia Jeshi la Magereza ili kuona kwamba tunaongeza Maafisa hawa ili watoto wetu waweze kupata huduma nzuri za kuweza kusaidiwa na Maafisa hawa pamoja na kwamba kuna nafasi nyingine ya kushughulikiwa na wazee wao na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine Mheshimiwa amegusia suala la kwa nini isipitiwe upya sheria au tuone namna, nimwambie kwamba sheria hii kwamba ipo vizuri, lakini kwa kuwa na yeye ameshauri tuipitie upya basi tutakaa tutaipitia sheria hii ili kama kutakuwa kuna mapungufu basi tutajua namna ya kuifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ushauri huo wa kuipitia upya umepata kutoka kwa mtu mzoefu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge pia aliuliza umuhimu wa kujua idadi ya kesi za watoto. Kesi zote zinazokwenda Mahakamani zinasajiliwa kwa namba, kwa hiyo kama atauliza swali mahsusi kwa Mahakama maalumu au kwa Gereza maalum idadi hiyo itapatikana kwa namba na kwa majina ya wahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili; Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inaweka misingi ya kulinda maslahi ya mtoto. Kwa hiyo, kwa mtu aliyechini ya kizuizi cha magereza anapopelekwa mahakamani kama hapati huduma inayostahili akiwa magereza anayohaki ya kutoa hiyo hoja kwa Hakimu ambapo shauri hilo lipo mbele yake na maelezo ya kisheria kwenda kwa wanaosimamia hizo *selo* yakatolewa. Nninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kweli nisipompa Balozi wa Magereza humu ndani swali la nyongeza. Mheshimiwa Esther Matiko, tafadhali.*(Kicheko)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali. Katika kulinda haki za watoto ni lazima au ni sharti tuzingatie wale watoto ambao unakuta hawana kesi, bali mama zao aidha wameenda wakiwa wajawazito au wamekamatwa ni mahabusu au mfungwa akiwa na mtoto ambaye yuko chini ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, katika Gereza la Segerea tumeshuhudia wamama wanakuja na watoto wao pale wa jinsia tofauti, lakini wanachangamana na watu wazima. Kwa hiyo, unakuta mtu mzima labda anataka kwenda kuoga anavua nguo, yuko hivi na mtoto yuko pale. Tunajua kwamba makuzi ya watoto ubongo wao ni kuanzia miezi sifuri mpaka miaka mitano. Kwa hiyo, unakuta unam-*affect* kisaikolojia.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua sasa, ni hatua gani Serikali inachukua kuhakikisha kwamba wale mahabusu au wafungwa ambao wamekwenda wakiwa wajawazito, wamejifungua wakiwa Magereza au wameenda na watoto wachanga, waweze kutengwa kwenye *cell special* ya akina mama wenye watoto au wajawazito wasiweze kuchangamana na hawa watu wengine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu ya swali hilo muhimu la kijinsia.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna hatua nyingi ambazo huwa zinachukuliwa. Huo utaratibu upo na upo tangu zamani. Inawezekana tu labda kuna maeneo yeye ameyashuhudia, ameona kwamba watu wanachanganyika na wengine wanakuwa wanataka labda pengine... kama hivyo. Kikubwa nimwambie kwamba ziko hatua ambazo Serikali inazichukua ikiwemo ya kuwatenganisha ili sasa ikitokea hali kama hiyo, waweze kupatiwa msaada maalum. Ziko hatua nyingi tu ambazo tunazichukua kama Serikali na kama Jeshi la Magereza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nahukuru sana. Tuendelee na Wizara ya Maji Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, uliza swali lako.

Na. 85

**Mradi wa Maji Lukululu**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kuendeleza Mradi wa Maji wa Lukululu ili kumaliza tatizo la maji katika vijiji 14 vya Jimbo la Vwawa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Lukululu unatekelezwa kwa awamu ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya kujenga miradi ya maji katika vijiji vitano kati ya 15 vya Mradi wa Maji Lukululu ambavyo ni Myovizi, Mbewe, Mahenje, Mlangali na Ndolezi. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa matanki manne ambapo kwa pamoja yatahifadhi maji lita 450,000 na mtandao wa mabomba wa urefu wa kilomita 58.3. Kazi hii itaanza kutekelezwa mwezi Desemba, 2021.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili itahusisha Vijiji 10 ambavyo ni Mbulu, Ivugula, Igunda, Ichesa, Shaji, Shomola, Shidunda, Ilea, Mbwewe na Lukululu. Kazi ya usanifu imepangwa kukamilika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/2022 na matarajio ni kupatikana Mkandarasi na utekelezaji utaanza Julai, 2022.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi za Serikali zinalenga kuboresha huduma ya upatikanaji majisafi na salama Wilayani Mbozi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, nimekuona.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Naomba nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya mradi huu ambao ni wa muda mrefu. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika awamu ya kwanza inahusu vijiji vitano; na kwa kuwa maji haya yanatoka

katika Kijiji cha Lukululu ambao ndio wanalinda hata vyanzo vya maji, lakini hawapo katika awamu ya kwanza; na kwa kuwa maji yanapotoka Kijiji cha Lukululu yanakuja Mlangali yanakwenda Shaji na Mahenje, lakini Kijiji cha Shaji ambacho kiko katikati hakiko katika mpango huu wa kwanza:-

Je, atakuwa tayari kubadilisha huu mpango ili hivi vijiji viwili, cha Lukululu ambako maji yanatoka na kile cha Shaji viwepo katika awamu ya kwanza? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili: Kwa kuwa Mbewe umeitaja na imeandikwa kwenye maeneo mawili; kwenye mpango awamu ya kwanza na awamu ya pili; sasa kuna kijiji ambacho kimesahaulika kilitakiwa kiingie katika vile vijiji kumi vya awamu ya pili, ambacho ni Ihoa:-

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kukiingiza hicho kijiji ili nacho kiwemo katika orodha ya vijiji vitakavyopata maji? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hasunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa Vijiji hivi vya Lukululu na Shaji sifa yake tu namna ambavyo ipo inafaa kuingia kwenye awamu ya kwanza, hivyo hatutakariri namna ambavyo tuliweka. Kwanza, Sera ya Maji inatutaka kijiji kile ambacho chanzo kipo kiwe mnufaika namba moja, hivyo tutazingatia hilo kama Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na maji kufika Ihoa, hii nayo nimeipokea. Kwa kuwa nia njema, dhamira safi ya Mheshimiwa Rais ni kuona kwamba maeneo yote yanafikiwa na huduma ya maji safi na salama, tutafikisha maji Ihoa pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda, tunaendelea na Wizara Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza swali langu naomba kufanya marekebisho ya hili jina. Badala ya kusema neno Igumbi, isomeke Igurubi kwenye *Hansard*.

Na. 86

**Kuipandisha Hadhi Barabara ya Igurubi – Igunga**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi barabara ya Igurubi – Mbutu – Igunga hadi Itumba yenye zaidi ya km 140 kuwa chini ya *TANROADS* ili ijengwe kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Marekebisho hayabadilishi maudhui ya swali. Majibu ya swali hilo tafadhali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, nimeshakuona Mheshimiwa Mhandisi Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, taratibu za kupandisha hadhi barabara ni kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za Mwaka 2009. Kwa vile suala hili ni la kisheria, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge awasilishe maombi yake ya kupandisha hadhi Barabara ya Igurubi – Mbutu – Igunga – Itumba, yenye kilometa 102.8 kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Tabora. Bodi ya Barabara ya Mkoa itajadili maombi hayo na ikiridhia

itawasilisha maombi kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambaye ndiye mwenye dhamana ya kupandisha hadhi ya barabara nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa, nimekuona.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumwambia Naibu Waziri kwamba tulishapeleka maombi na Serikali ilituma wataalam wakafanya *survey* mwaka 2013/2014, lakini pia na mwaka 2016 walikuja wakafanya *survey* wakawa wamewasilisha Wizarani.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia barabara hii ndiyo kiunganishi cha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Simiyu ambao kimamlaka ulitengenezwa mwaka 2012.

Kwa hiyo, namwomba Waziri aweze kulipa kipaumbele, walifikirie ombi letu na waweze kuipandishwa hadhi ijengwe kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, una la kusema kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kupokea ushauri wa Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, kama alivyoomba.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie kwamba kama limeshafika Wizarani, basi tutaliangalia tuone kama limekwama; na kama kuna vigezo ambavyo vinashindikana, basi nitaomba tuwasiliane naye ili kama kuna shida tuone. Kama inakidhi vigezo vyote, nadhani barabara hii itapandishwa hadhi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge wa Mtambwe, Mheshimiwa Khalifa, uliza swali lako.

Na. 87

**Umuhimu wa Marubani Wawili Katika Ndege**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha uwepo wa marubani wawili kwenye ndege ndogo za abiria?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Bado tupo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ndege zote kwa mujibu wa vyeti vya utengenezaji *(type certificate)* huwa zina taarifa inayoelekeza mambo muhimu ya kifundi na usalama yahusuyo operesheni za ndege hizo. Pamoja na hizo nyaraka mbili, pia kuna kitabu cha maelekezo ya matumizi. Ndege zote zenye uzito wa kilogramu 5,700 kwenda chini ni ndege za rubani mmoja kwa mujibu wa nyaraka za mtengenezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga na Sheria ya Kimataifa ya Usafiri wa Anga, haizuii ndege hizo kuendeshwa na rubani mmoja na ni salama kufanya hivyo. Hata hivyo, nchi yetu imeweka sheria ya kuwa na marubani wawili kwa ndege yoyote ya abiria yenye uzito unaozidi *kilogram* 5,700 hata kama mtengenezaji wake anaruhusu rubani mmoja mmoja, katika kujiwekea wigo mpana wa kuweka usalama wa anga.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeweka utaratibu wa kuhakiki afya za marubani mara kwa mara kwa mujibu wa sheria. Uhakiki wa kati na mkubwa

hufanyika kila baada ya miezi sita kwa marubani wenye umri unaozidi miaka 40 na kila baada ya miezi 12 kwa marubani wenye umri wa chini ya miaka 40. Uhakiki wa mara kwa mara na wa kushtukiza pia hufanyika. Aidha, rubani yeyote anayekutwa na changamoto za kiafya huwekewa sharti la kutoruka peke yake au kuzuiwa kuruka kabisa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtabwe, swali la nyongeza.

**MHE. KHLAIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Waziri kwa majibu yake ya kina, lakini hata hivyo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu lilihusu hasa usalama wa raia wanaporushwa katika ndege. Usalama wao huu siyo kwa sababu ya uchache na udogo wa ndege. Ndege nyingi takribani ndogo ndogo hizi ambazo tunaruka nazo ni chini ya kilogramu 4,000, lakini bado ni abiria: Je, Serikali itabadilisha sheria hata kuwa ndege ni ya watu watatu, kilogram 3,000 kuleta marubani wawili?

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu marubani kufanyiwa uhakiki wa afya zao miezi sita au 12; mgogoro wa afya unaweza kutokea wakati wowote akiwa ndani ya anga. Sasa unaonaje, unanusuru vipi abiria wale ambao rubani wao amepata changamoto ya afya akiwa angani peke yake? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalifa, Mbunge wa Mtambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Mbunge anataka kujua, ni kwa nini ndege ambazo zinabeba watu chini ya kilo 3,000 haziwezi kutumia marubani wawili?

Kwanza, ndege inapokuwa inatengenezwa, yule mtengenezaji anatoa maelekezo marubani wangapi wanapaswa kuitumia hiyo ndege.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni kweli kwamba kutumia marubani wawili kwenye ndege moja ndogo pia ni gharama, maana yake huyo rubani inabidi alipwe. Ila sisi kisheria tumeruhusu kwamba unaweza ukatumia marubani wawili, lakini waendeshaji wadogo kwenye ndege zao hawazuiliwi kisheria kutumia marubani wawili.

Mheshimiwa Spika, la tatu, wanaangalia pia ile ndege aina ya mitambo na vipuri vinavyotumika. Ndege hizi ndogo zinabeba chini ya abiria 19 na haziendi umbali mrefu zaidi na hazitembei kwa saa nyingi na haziendi juu ya anga kwa maana ya kupata mikikimikiki ile ya mawimbi makubwa. Hata hivyo ikitokea kuna viashiria vya hali ambayo siyo nzuri kwa afya, kwa kuchukua tahadhani wanaweza kuongeza rubani wa pili katika ndege hiyo.

Mheshimiwa Spika, la pili ni uhakiki wa afya za marubani kwamba wale ambao wana miaka chini ya 40 ni mizei sita, lakini wale zaidi ya miaka 40 ni miezi 12. Hii ni ukweli kwamba kisayansi kwa mazoea ni kwamba hawa wenye chini ya miaka 40 ni vijana, tunaamini kwamba wana afya na nguvu ya kuweza kufanya kazi zaidi. Ila ikitokea kwamba kuna viashiria vya hali ya usalama kiafya wanaweza kufanyiwa utaratibu wa kupimwa afya zao hata chini ya miezi mitatu. Ni jambo ambalo linawezekana.

Mheshimiwa Spika, tunafanya mambo yote haya kwa kuzingatia Sheria ya Anga ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa, hii siyo kwa marubani tu, hii ina-*apply* kwa maisha ya kawaida ya sisi wote. Miezi sita kwa wale wenzangu mimi na wale wengine, kila baada ya mwaka angalau kufanya *checkup* kubwa ya afya.

Swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

Na. 88

**Ujenzi wa Barabara ya Nzera – Nkome**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara yenye urefu wa kilometa 20 kutoka Nkome hadi Nzera?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nzera – Nkome ni sehemu ya Barabara ya Geita – Nzera hadi Nkome yenye urefu wa kilometa 54 inayounganisha Mji wa Geita ambayo ni Makao Makuu ya Mkoa na Miji Midogo ya Nzera, Nkome na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuandaa makabrasha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina Barabara yote kutoka Geita – Nzera hadi Nkome (kilometa 54) kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 2,000 kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi. Baada ya usanifu kukamilika na gharama

za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea na maandalizi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iweze kuendelea kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 1,162 zimetengwa kwa kazi hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, nimekuona.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Barabara inayotoka Geita kwenda Nkome ina kilometa 57 na ilishafanyiwa upembuzi yakinifu muda mrefu na ikawekwa mpaka *beacon* na alama za kuanza mkandarasi. Leo tunazungumza ni karibia mwaka wa pili, tunaahidiwa kila siku: Ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja kuuona Mji wa Nzera ambao ndiyo Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Geita; haijawahi kuona lami; kila mwaka tunaahidiwa na leo ni mwaka wa nne?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Barabara ya Kamanga – Sengerema – Buchosa – Nkome ni barabara ambayo imeng'oa Wabunge zaidi ya sita, upande wa Sengerema na upande wa Buchosa; lakini tumekuwa tukipata ahadi zilezile za Serikali kwamba mwakani tunajenga, mwakani tunajenga; sasa nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri, tufundishe njia ambayo unaona ni nzuri na sisi tupite kama ni dirishani angalu tupate hiyo lami. Bado tunapenda kuendelea kuwa Wabunge.

Naomba *commitment* ya Serikali, ni lini mtaanza kutengeneza Barabara ya Kamanga – Sengerema – Buchosa – Nkome?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *beacon* zilizowekwa haikuwa usanifu wa kina; na fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya mwaka huu tunaoutekeleza inakwenda kufanya kazi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, yako maandalizi ambayo yanaendelea kwa ajili ya kuanza huo mchakato wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina yakiwa ni maandalizi ya kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya pili aliyoisema ya Kamanga – Sengerema – Buchosa hadi Nkome, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba itatekelezwa kama ilivyoahidiwa kwenye Mpango wetu na kama ilivyoelezwa kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2020 - 2025. Pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kutafuta fedha na ikipatikana hizi barabara zote zitajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umeisha na maswali yamekwisha pia. Sasa naendelea na matangazo ambapo nina wageni wanne kwenye Jukwaa la Spika. Hao wageni wanne wanatoka *Stanbic Bank,* wakiongozwa na Mkurugenzi wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Ndugu Omay Mtiga. Ahsante sana wageni wetu kutoka *Stanbic Bank. Stanbic Bank* wapo katikati ya Mji pale, wanapaita Uhindini na huduma zao ni nzuri, tuwatembelee kila tunapopata nafasi. *(Makofi)*

Pia wapo Mkuu wa Kitengo cha Wateja Maalum, Ndugu Edditrice Marco; Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Ndugu Ruth Mwaiselage; Mkuu wa Tawi la Dodoma, Ndugu Oppi Igolola; karibuni sana *Ma-bankers* wetu wa *Stanbic*

*Bank.* Wana *package* maalum wanaomba sana muwatembelee. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, ambao ni wapigakura wake kutoka Jijini Tanga. Wakiongozwa na Ndugu Mwajuma Mohamed, karibuni sana, karibuni sana wageni wetu kutoka Tanga. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Nusrat Hanje, ambao ni wadau wa masuala ya habari na viongozi wa *The Media Institute of Southern Africa (MISA),* wakiongozwa na Kaimu Mkurugenzi *MISA Tanzania*, Ndugu Andrew Marawiti, karibuni sana *MISA*. *(Makofi)*

Wageni 70 wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, ambao ni wanafunzi wa Diploma ya Maendeleo ya Jamii mwaka wa pili kutoka Chuo cha Mipango cha Jijini Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Gerald Swai. Chuo cha Mipango karibuni sana sana. Karibuni sana ndugu zetu kutoka Mipango. *(Makofi)*

Pia tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, ambao ni wapigakura wake kutoka Liwale Mkoani Lindi, Ndugu Jaizu Mkinde, Haji Nginja na Pascal Sarme. Karibuni sana natumaini mmetoka Liwale moja kwa moja kuja Dodoma, basi mtupelekee salamu kule Mtawatawa, Barikiwa, Pigamiti, Makunjiganga, Nangano, Kimambi mpaka Ndapata kule mwisho kule kote mpeleke salamu.

Mheshimiwa nikija kugombea huko utapata taabu, Liwale nyumbani pia mimi. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka, 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.6 Bill, 2021)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite mtoa hoja. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge naomba tumsikilize Mwanasheria Mkuu wa Serikali akiwasilisha hoja hii mbele yetu na niwaombe tuwe wavumilivu, leo tunamaliza mapema tu wala tusiwe na wasiwasi. Mheshimiwa *AG*. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka, 2020, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka, 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.6 Bill, 2021)* kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho, sasa usomwe kwa Mara ya Pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia neema zake na kutuwezesha kukutana katika Mkutano wa Tano wa Bunge hili Tukufu. Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuniteua mnamo tarehe 12 Septemba, 2021 na kuniapisha kushika nafasi hii ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mnamo tarehe 13 Septemba, 2021. Namwahidi kutekeleza majukumu yangu haya mapya kwa weledi, umahiri na uaminifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Mheshimiwa Phillip Isidori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Pili, namshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama kwa mara ya kwanza mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka, 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2021)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge na Katibu wa Bunge kwa kutuongoza na kusimamia vyema vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa weledi na kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Kwa namna ya kipekee, naomba uridhie nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu na Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato na timu zao za wataalam kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika hatua zote za maandalizi na uchambuzi wa Muswada huu mpaka kufikia hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga Sheria, pamoja na kuisimamia Serikali na pia kunipatia ushirikiano wa kutosha tangu uniapishe kuwa Mbunge mnamo tarehe 2 Novemba, 2021.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao

ulisimamiwa kwa karibu sana na Bwana Onorius J. Njole, ambaye ni Mwandishi Mkuu wa Sheria, akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam kutoka kwenye Wizara ambazo tulishirikiana nao. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka, 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.6 Bill, 2021)* ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, napenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wote wa kupitia Muswada huu katika Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada na kuishauri Serikali kuuboresha. Matokeo ya mashauriano kati ya Serikali na Kamati yanajidhihirisha katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali kama yalivyowasilishwa, ambapo sasa Serikali inapendekeza kufuta na kuandika upya Ibara ya 6 ya Muswada na kufuta Sehemu ya Nne ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka, 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.6 Bill,* 2021) kama ulivyowasilishwa unapendekeza Marekebisho katika Sheria zifuatazo:-

(i) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;
(ii) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438; na
(iii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne ambapo Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la Sheria inayopendekezwa na Tamko la Marekebisho

ya Sheria Mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa Marekebisho kupitia Muswada huu.

Sehemu ya Pili ya Muswada, inapendekeza Marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, ambapo Kifungu cha 83(b) kinapendekezwa kufutwa kwa lengo la kuondoa kodi ya zuio la asilimia mbili kwenye mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Lengo la Marekebisho haya ni kulinda vipato vya wakulima kwa kuwapunguzia mzigo unaotokana na utozwaji wa kodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada, ikisomwa pamoja na Jedwali la Marekebisho ya Serikali, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 ili kurekebisha Kifungu cha 7 na kuongeza kifungu kidogo cha (3). Marekebisho haya yanalenga kutambua Mkataba wa Utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka *Hoima* nchini Uganda kwenda Chongoleani, Tanga ili utekelezaji wa Sheria za Kodi usiathiri masharti mahususi ya Mkataba huo kama ilivyokubaliwa na pande mbili husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali na kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali Sehemu ya Nne ya Muswada, inayopendekeza Marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 inapendekezwa kufutwa. Hatua hii inatokana na mashauriano ya kina kati ya Serikali na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, naomba Bunge lako Tukufu, liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka, 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.6 Bill, 2021)* na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

# THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 6) ACT, 2021

## ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*


PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short Title.
2. Amendment of certain written laws.

PART II
AMENDMENT OF THE INCOME TAX ACT,
(CAP. 332)

3. Construction.
4. Repeal of section 83B.

PART III
AMENDMENT OF THE TAX ADMINISTRATION ACT,
(CAP. 438)

5. Construction.
6. Addition of section 7A.

PART IV
AMENDMENT OF THE VALUE ADDED TAX ACT,
(CAP. 148)

7. Construction.
8. Amendment of section 6.
9. Amendment of section 11.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

## NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
30th October, 2021

**HUSSEIN A. KATTANGA**
*Secretary to the Cabinet*

**A Bill**
*for*

**An Act to amend certain written laws.**

**ENACTED** by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short Title

**1.** This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6) Act, 2021.

Amendment of certain written laws

**2.** The written laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts.

PART II
AMENDMENT OF THE INCOME TAX ACT,
(CAP. 332)

Construction Cap. 332

**3.** This Part shall be read as one with the Income Tax Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Repeal of section 83B

**4.** The principal Act is amended by repealing section 83B.

PART III
AMENDMENT OF THE TAX ADMINISTRATION ACT,
(CAP. 438)

Construction Cap. 438

**5**. This Part shall be read as one with the Tax Administration Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Addition of section 7A

**6**. The principal Act is amended by adding immediately after section 7 the following:

"Application of tax laws in agreement with special arrangement

**7A**.-(1) Where an agreement provides for special arrangement relating to tax laws and the said agreement has been approved by the Cabinet, the application of such tax laws shall not prejudice the implementation of such agreement to the extent of such arrangement.

(2) The provisions of subsection (1) shall apply to an agreement for implementation of strategic project of which the Government is a party.

(3) An agreement under this section shall provide for the type, scope and the beneficiary of such arrangement.

PART IV
AMENDMENT OF THE VALUE ADDED TAX ACT,
(CAP. 148)

Construction Cap. 148

**7**. This Part shall be read as one with the Value Added Tax Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 6

**8.** The principal Act is amended in section 6,

(a) in subsection (2) by adding at the end of paragraph (a) the words "and LPG Cylinders"; and

(b) in subsection (7) by inserting the words "and LPG Cylinders" between the words "nets" and "having".

Amendment of section 11

**9**. The principal Act is amended in section 11(10) by inserting the words "and HS code 8716.31.10, 8716.31.90, 8716.39.10, 8716.39.90, 8716.40.10, 8716.40.90" between the words "and 90" and "of annex".

## OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes amendments to Three laws, namely; Income Tax Act, (Cap. 332), the Tax Administration Act, (Cap. 438) and the Value Added Tax Act, (Cap. 148).

The Bill is divided into Four Parts.

Part I deals with preliminary provisions which include the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended, are amended in their respective Parts.

Part II of the Bill proposes amendment to the Income Tax Act, Cap. 332 by repealing section 83B with the aim of removing the two percent withholding tax on agricultural, fishery and livestock products. The proposed amendment intends to protect farmers who have been affected by the income tax deducted from farmers' produce.

Part III of the Bill proposes to amend the Tax Administration Act, Cap. 438 by adding a new section 7A that requires tax laws to be applied without prejudicing agreements that have been approved by the Cabinet. The proposed amendments intend to provide smooth and expeditious implementation of agreements entered by the Government that provides for the execution of special arrangements, and to create favourable conditions for performance of Government projects.

Part IV of the Bill proposes to amend the Value Added Tax Act, Cap. 148 where section 6 is amended to provide for VAT exemption on imported raw materials used to manufacture natural gas cylinders. The aim of the amendment is to stimulate the domestic use of natural gas in compliance to the Paris Agreement Treaty on Climate Change (COP-21) which provides for reduction of global warming. Furthermore section 11 is amended to allow deferment tax on trailer manufacturing industries in order to promote investments.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tatu zifuatazo; Sheria ya Kodi ya Mapato, (Sura ya 332); Sheria ya Usimamizi wa Kodi, (Sura ya 438) na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, (Sura ya 148).

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi na yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho zimerekebishwa katika Sehemu husika ya Muswada.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 kwa kufuta kifungu cha 83B kwa lengo la kuondoa kodi ya zuio ya asilimia mbili kwenye mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Lengo la marekebisho haya ni kuwalinda wakulima ambao wameathirika kutokana na kodi husika kukatwa kwenye mazao yao badala ya kodi hiyo kulipwa na wafanyabiashara wa mazao kama ilivyokusudiwa.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 kwa kuongeza kifungu kipya cha 7A kinachoelekeza kwamba matumizi ya Sheria za Kodi yasiathiri mikataba iliyoridhiwa na Baraza la Mawaziri ambayo ina masharti maalum. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora na wa ufanisi wa miradi mbalimbali ambayo Serikali imeingia na ambayo ina masharti maalum ya kikodi.

Sehemu ya Nne inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 ambapo kifungu cha 6 kinarekebishwa ili kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani yaani VAT kwenye malighafi zinazotumika kutengenezea mitungi ya gesi asilia zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea matumizi ya gesi asilia majumbani ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa masharti ya Mkataba wa Kimataifa wa Paris (COP-21) wa kupambana na athari ya kimazingira duniani. Vile vile kifungu cha 11 kinafanyiwa marekebisho ili kuwezesha viwanda vinavyotengeneza matrela nchini kunufaika na ahirisho la kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye uuzaji wa bidhaa husika.

Dodoma,
29 Oktoba, 2021

**ELIEZER M. FELESHI**
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. DR. ELIEZER MBUKI FELESHI, THE ATTORNEY GENERAL AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 6) ACT, 2021"**

*(Made under SO.O. 99 (10))*

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 6) Act, 2021" is amended as follows:

**A:** By deleting Clause 6 and substituting for it the following:

"Amendment of Section 7

**6.** The principal Act is amended in section 7 by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) For purposes of this section, the Host Government Agreement concerning the East Africa Crude Oil Pipeline (EACOP) Project shall be regarded as an international agreement and the provisions of subsection (1) shall apply.".

**B:** By deleting the whole of Part IV.

Dodoma,

…………………….., 2021

**EMF**
*AG*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nawashukuruni sana, nakushukuru sana Mheshimiwa *AG* kwa kuwasilisha kwa umahiri mkubwa hoja hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, nina mambo mawili ambayo nilitakiwa niyatangaze wakati ule kabla, hivyo sijamwita Mwenyekiti wa Bajeti naomba niyatangaze.

La kwanza, Mheshimiwa Mbunge Francis Mtega wa Mbarali aliwahi kuleta maelezo yake humu Bungeni (malalamiko) ya suala la vijiji vya kule Mbarali. Naamini Kamati ya Waheshimiwa Mawaziri labda *I am not sure* itakuwa labda imepitapita huko katika kipindi hiki lakini inaelekea kama Mheshimiwa bado ana *grievance* kubwa kuhusu jambo hilo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili nalielekeza kwa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwenye kipindi kinachokuja kwenye shughuli za Kamati, nitawapa kibali kwenda Mbarali, mkafanye mikutano kule, mtuletee *respective* ya Wabunge ili tuweze na sisi kuishauri Serikali kuhusu jambo hili kwa sababu, limekuwa sugu sana kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, Kamati ya Ardhi mkumbuke kwenye ratiba yenu ile ya wakati ule, mtukumbushe muweze kwenda Mbarali. Baadaye tuje *tu-compare notes* zetu na Serikali endapo na wao watakuwa walishaenda huko. *(Makofi)*

Jambo la mwisho, yuko ndugu yetu mmoja ni Mzee maarufu anaitwa Jenerali Ulimwengu. Huyu Mzee hivi karibuni amekuwa akiropokaropoka sana na anazivunjia heshima Taasisi mbalimbali na watu mbalimbali lakini kinachotugusa sisi amekuwa akilivunjia heshima Bunge hili na Spika pia. Sasa kwa sababu, ni mtu mzima, ni msomi mwelewa, *tuna-assume* anafanya makusudi. Sasa kwa sababu anafanya makusudi, ningependa nitumie nafasi hii kumpa onyo kali huyu mzee

kuchunga ulimi wake. Haipendezi mtu wa umri wake na uzoefu wake kuwa anaongea hovyo hovyo, anakashifu kashifu watu haipendezi. *(Makofi)*

Sasa cha kusema ni kwamba, akiendelea basi na sisi tutaacha ukimya, itabidi watu washughulike naye kwa *front* zote ikiwemo Bungeni, ikiweko Mahakamani na mahali pengine ambako naamini tu atapata tabu sana. Kwa sababu, yuko *so lose* katika kukashifu na kudharau watu, tabu sana. Basi habari imfikie kwamba uvumilivu wetu umefika mwisho, akiendelea tena na mambo yake basi tutaona nini cha kufanya. *(Makofi)*

Sisi sio kama anavyodhani wala sisi sio mazuzu, wala sio kama anavyofikiri yaani ana maneno ya rejareja mengi sana, ya hovyo hovyo sana. Kiswahili rahisi anatukadiria yaani, hajatupima uzito wetu anakadiria kadiria tu, sisi sio uzito huo anaofikiri, ningependa kuchukua nafasi hii. *(Makofi/ Kicheko)*

Baada ya maneno hayo, naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti atupitishe katika hotuba yake ya mapitio ya kazi hii nzuri ambayo Bajeti wameifanya.

Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti, karibu sana kwa hotuba ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. OMARI M. KIGUA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Mabadiliko wa Sheria Mbalimbali Na.6 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.6).*

Mheshimiwa Spika, Utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2020, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka, 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments), No.6)*.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Novemba, 2021, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi na Ajira aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na.6. Baada ya kuwasilisha Muswada huo, uliagiza Kamati ya Bunge ya Bajeti kuuchambua Muswada huo. Siku hiyo hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasilisha Mapendekezo hayo mbele ya Kamati ya Bajeti kwa niaba ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Muswada; Kamati kwa muda wa siku mbili ilifanya vikao kwa ajili ya kuuchambua Muswada huo uliowasilishwa mbele ya Kamati wakati wa Vikao vya Bunge vikiendelea kama ulivyoagiza. Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada tarehe 10 Novemba, 2021, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri wa Nishati, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka, 2021; Muswada huu unafanya mabadiliko katika Sheria Tatu za Kodi ambazo ni Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 338 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*, Sura ya 138. Baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati na Serikali Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 *The Income Tax Act, Cap*. 332; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kufuta Kifungu cha 83(b) ambacho kilianzisha Kodi ya Zuio ya asilimia mbili *Withholding Tax* kwenye mauzo ya mazao ya kilimo, uvuvi, mifugo na kwa makampuni yaliyosajiliwa. Ieleweke wazi kwamba

mabadiliko haya ni utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka, 2021 na baadaye Sheria ya Fedha ya Mwaka, 2021. Kwa sababu hiyo ni vyema Serikali ikatambua umuhimu wa kusikiliza maoni na ushauri wa Kamati utolewao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina Kamati ilikubaliana na Serikali kuboresha kifungu cha 7 cha Sheria ya Utawala wa Kodi kwa kuongeza kifungu kidogo cha 3 ili kutanzua vikwazo vya kisheria vilivyokuwa vinakwamisha utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima hadi Chongoleani Tanga.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi Ongezeko la Thamani Sura 248 *(Value Added Tax Act Cap. 248)*; baada ya majadiliano baina ya Kamati na Serikali, Serikali ilikubali kuondoa mapendekezo hayo kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya ujumla, Masuala mengine yaliyojadiliwa katika Kamati wakati wa kupitisha Muswada wa sheria wa fedha ni kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, vifungashio kwa ajili ya madawa yanayozalishwa nchini, kamati inaishauri Serikali kwamba kuna haja ya kufanya mabadiliko ya haraka ya kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifungashio vya dawa, mfano hivi sasa chupa za kutengeneza *drip* na karatasi za kufungia dawa zinazotozwa kodi ya *VAT*, hatua hii inaathiri kiwanda cha uzalishaji wa madawa ya *MSD* na inaathiri kiwanda chengine kimpya cha *MSD* kinachojengwa katika Mkoa wa Njombe, hatua hii itachochea uzalishaji wa dawa nchini na kwa bei nafuu kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utendaji wa kazi wa *task force on taxes reforms* na mapendekezo ya kamati kuhusiana na masuala ya kodi. Kamati imebaini kwamba kuna changamoto katika utendaji wa kazi wa kikosi cha kujadili

kubadili ya kodi, kwa sababu mabadiliko haya yalisuluhishwa kwenye kikosi kazi na hayakupitishwa. Hivyo ni wazi kwamba Serikali haikuchukua maoni, ushauri, ushauri na mapendekezo ya wadau kuhusiana na masuala ya kikodi, hivyo kamati inaishauri Serikali izingatie maoni ushauri na mapendekezo ya wadau kuhusu ya kodi yenye tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Ofisi ya Mpokea Malalamiko ya Walipo Kodi *(Tax of Ombudsman);* Kamati imekuwa ikishauri Serikali kutekeleza mara moja mabadiliko yaliyofanyika kwenye sheria ya usimamizi wa kodi mwaka 2018 sura 438 na kuanzishwa ofisi ya mpokea malalamiko ya kodi. Hadi sasa Serikali haijaanzisha ofisi hiyo miaka tatu tangu sheria hiyo ipitishwe bungeni. Kamati inaamini uwepo wa ofisi hiyo utasaidi kwa kiasi kikubwa kupunguza malalamiko ya kodi. Aidha, kamati inaitaka Serikali hadi kufikia mwezi wa nne mwaka 2022 ofisi hii iwe imeanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kuimarisha vitengo vya utafiti wa sera za mapato ili kuiwezesha Serikali kuwa na taarifa za uhakika pindi inapoandaa zera za mapato. Kuna haja ya msingi ya kuimarisha vitengo vya utafiti wa sera za mapato na hasa kodi kwa kuvitengea rasilimali watu na fedha za kutosha ili kuvitekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inaami mabadiliko yanayofanywa mara kwa mara katika sheria za kodi ni kutokana na kutokuwa na utafiti wa kina katika sera za mapato. Serikali ifanye utafiti na tathmini wa misamaha ya kodi endapo inafikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi ni hatua za sera za mapato ambayo huwa na malengo mbalimbali kama vile kuchochea uzalishaji, kupunguza gharama za huduma au bidhaa, kugawanya rasilimali na kuchochea ukuwaji wa sekta. Hata hivyo malengo tuliyojiwekea katika mpango wa miaka tano misamaha haitakiwi kuzidi asilimia moja ya pato la Taifa. Hivyo ni wakati sasa umewadia kwa Serikali kufanya tathmini ya kina ya misamaha yote ya kodi iliyotolewa na kuona endapo misamaha hiyo imefikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, naomba kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya kamati kuhusu Muswada ya mabadiliko ya sheria mbalimbali Na. 6 mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, pili nimshukuru Mheshimiwa Dkt Tulia Ackson Mbenge Naibu Spika kwa ushirikiano wake. Aidha, napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Stephen Byabato Mbunge Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Eliezer Feleshi, Mbunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Nishati pamoja na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maoni na ushauri uliowezesha kamati kuuchambua Muswada hadi kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wote wajumbe wa kamati ya bajeti kwa umakini, umahiri, utulivu na uvumilivu wao wakati wa kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu, hasa ukuzingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana, naomba nisitaje majina yao.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndugu Michael Kadebe - Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono, ahsante. *(Makofi)*

# MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA 6 *(THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMMENDMENTS) (NO.6)* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2020 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na 6 wa mwaka 2021 **The Written Laws (Miscellaneous Ammendments) (No.6**)

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 09 Novemba, 2021, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Kazi na Ajira aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na 6 na baada ya kuwasilisha Muswada huo, Mheshimiwa Spika uliiagiza Kamati ya Bunge ya Bajeti kuuchambua muswada huo. Siku hiyo hiyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasilisha Mapendekezo hayo mbele ya Kamati ya Bajeti kwa niaba ya Serikali.

### 1.1. Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa muda wa siku mbili ilifanya vikao kwa ajili ya kuuchambua Muswada huo uliowasilishwa mbele ya Kamati wakati vikao vya Bunge vikiendelea kama ulivyoagiza.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada, tarehe 10 Novemba, 2021 Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri wa Nishati, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Nishati.

## 2.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MABADILIKO YA SHERIA MBALIMBALI NA 6 WA MWAKA 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unafanya mabadiliko katika sheria tatu za Kodi ambazo ni Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332, Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) Sura ya 148. Baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati na Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo: -

### 2.1. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 (*The Income Tax Act, (Cap 332*)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na Mapendekezo ya Serikali ya kufuta Kifungu 83B ambacho kilianzisha kodi ya zuio asilimia 2 (withholding tax) kwenye mauzo ya mazao ya Kilimo, uvuvi, mifugo na kwa makampuni yaliyosajiliwa. ieleweke wazi kwamba mabadiliko haya ni utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021, na baadaye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021. Kwa sababu hiyo ni vyema Serikali ikatambua umuhimu wa kusikiliza maoni na ushauri wa Kamati mara utolewapo.

### 2.2. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438, (The Tax Administration Act, (Cap 438)

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufanya mabadiliko katika kifungu cha 7 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi kwa kuongeza Kifungu cha 7A kinachoweka masharti kwamba, matumizi ya Sheria za Kodi yasiathiri utekelezaji wa Mikataba kati ya Serikali na makampuni au taasisi nyingine iliyoridhiwa na Baraza la Mawaziri na yenye nafuu ya kodi. Kwa mujibu wa Madhumuni ya Muswada, lengo la mapendekezo haya ni kuwezesha utekelezaji bora na wenye ufanisi wa miradi mbalimbali ambayo Serikali imeingia mikataba na ina masharti maalumu ya kikodi.

**Mheshimiwa Spika,** Baaada ya majadiliano ya Kina Kamati ilikubaliana na Serikali kuondoa mapendekezo ya kuongeza kifungu cha 7A na badala yake kuboresha kifungu cha 7 cha

Sheria ya Utawala wa Kodi kwa kuongeza kifungu kidogo cha 3 ili kutanzua vikwazo vya kisheria katika utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima hadi Chongoleani Tanga. Mabadiliko yatakayohusu miradi mingine yote ya Mkakati yafanyike kupitia kifungu cha 20 cha Sheria ya Uwekezaji ili kuweka utaratibu utakaotumika kwa miradi ya kimkakati itakayokuwa.

**2.3. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 (*Value Added Act, (Cap 148*)**

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya majadiliano baina ya Kamati na Serikali, Serikali ilikubali kuondoa mapendekezo hayo kama inavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho.

## 3.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** masuala mengine yaliyojadiliwa katika Kamati wakati wa kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha ni kama ifuatavyo:

**3.1. Vifungashio kwa ajili ya madawa yanayozalishwa Nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwamba kuna haja ya kufanya mabadiliko ya haraka na kutoa msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye Vifungashio vya madawa. Mfano, hivi sasa chupa za kutengenezea *Drip* na karatasi za kufungia dawa zinatozwa kodi ya VAT. Hatua hii inaathiri hadi kiwanda cha uzalishaji wa Dawa cha MSD na itaathiri kiwanda kingine kipya cha MSD kinachojengwa katika Mkoa wa Songwe. Hatua hii itachochea uzalishaji wa Dawa nchini na kwa bei nafuu kuliko ilivyo hivi sasa.

**3.2. Utendaji wa Kazi wa *Task Force on Tax Reforms* na Mapendekezo ya Kamati kuhusiana na Masuala ya Kodi.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kuna changamoto katika utendaji kazi wa Kikosi kazi cha Kujadili mabadiliko ya Kodi, kwa sababu mabadiliko haya yaliwasilishwa kwenye kikosi kazi na hayakupitishwa. Hivyo ni wazi kwamba Serikali haikuchukuwa maoni, ushauri na mapendekezo ya Wadau kuhusiana na masuala ya kikodi. Hivyo Kamati inaishauri Serikali izingatie maoni, ushauri na

mapendekezo ya wadau kuhusu masuala ya kodi yenye tija kwa Taifa letu.

**3.3. Uanzishwaji wa Ofisi ya Mpokea Malalamiko ya Walipa Kodi "Tax ombudsman"**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutekeleza mara moja mabadiliko yaliyofanyika kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi Mwaka 2018 Sura ya 438 na kuanzisha Ofisi ya Mpokea Malalamiko ya Kodi. Hadi sasa Serikali haijaanzisha Ofisi hiyo miaka mitatu tangu Sheria hiyo ipitishwe na Bunge. Kamati inaamini uwepo wa Ofisi hiyo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza malalamiko ya Kodi. Aidha, Kamati inaitaka Serikali hadi kufikia mwezi wa nne mwaka 2022 Ofisi hii iwe imeanzishwa.

**3.4. Serikali kuimarisha Vitengo vya utafiti wa Sera za Mapato ili kuiwezesha Serikali kuwa na Taarifa za uhakika pindi inapoandaa sera za mapato.**

**Mheshimiwa Spika**, Kuna haja ya msingi ya kuimarisha vitengo vya utafiti wa Sera za Mapato na hasa kodi kwa kuvitengea rasilimali watu na fedha za kutosha ili vitekeleze majukumu yake kikamilifu. Kamati inaamini mabadiliko yanayofanywa mara kwa mara katika sheria za Kodi ni kutokana na kutokuwa na utafiti wa kina katika sera za mapato.

**3.5. Serikali ifanye utafiti na tathmini wa misamaha ya kodi endapo inafikia malengo yaliyokusudiwa.**

**Mheshimiwa Spika,** Misamaha ya Kodi ni hatua ya Sera za Mapato ambayo huwa na malengo mbalimbali kama vile kuchochea uzalishaji, kupunguza gharama za huduma au bidhaa, kugawanya rasilimali na kuchochea ukuaji wa sekta. Hata hivyo malengo tuliyojiwekea katika Mpango wa Miaka mitano misamaha haitakiwi kuzidi asilimia 1 ya pato la Taifa. Hivyo ni wakati sasa umewadia kwa Serikali kufanya Tathmini ya kina ya misamaha yote ya kodi iliyotolewa na kuona endapo misamaha hiyo imefikia malengo yaliyokusudiwa.

## 4.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kwanza kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na 6 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili nimshukuru Mhe Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika kwa ushirikiano wake. Aidha napenda nimshukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Stephen Byabato (Mb), Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Jaji Dkt. Elieza Feleshi (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Nishati pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi kufikia hatua hii.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashuruku Wajumbe wa kamati ya Bajeti kwa umakini, umahiri, utulivu na uvumilivu wao wakati wa kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu, hasa ukizingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana. Wajumbe hao ni:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| 17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb | Mjumbe |
| 20. Mhe. Halima James Mdee, Mb | Mjumbe |
| 21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. Dkt Charles Kimei, Mb | Mjumbe |
| 23. Mhe. Mariam Kisanji, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Bi Nenelwa Mwihambi, *ndc* pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Sillo Baran, (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**
11 Novemba, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kigua Makamo Mwenyekiti wa kamati ya bajeti, lakini kupitia kwako wajumbe wote wa kamati ya bajeti, tunawashukuruni sana kwa kazi kubwa. Tuliwapa kazi hii kwa muda mfupi kabisa lakini mmeifanya kwa bidii kubwa na mmekamilisha shughuli katika muda mfupi sana. Sasa tunaingia katika uchangiaji Mheshimiwa Riziki Lulida atuanzie kama yupo. Hayupo eeeh! Naendelea Mheshimiwa Joseph George Kakunda, na atafatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza napenda kupongeza sana sana Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali sana

watanzania. Baada ya kuwa malalamiko yamekuwa mengi ndani ya Taifa letu malalamiko yamefika kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais akaagiza kwamba sheria ambayo tulokuwa tumeipitisha mwezi wa 6 basi kile kifungu ambacho kilikuwa kinatoza asilimia mbili ya kodi ya zuio *(withholding tax)* kile kifungu kifutwe, kwa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni dalili moja wapo kwamba Serikali yetu inawajali wananchi pale ambapo zinatokeza changamoto Serikali inaitikia haraka kuweza kuondoa changamoto za aina kama hiyo. Mwanzoni wakati tunapitia sheria tulikuwa tumelenga kwamba watakaotozwa hiyo kodi yawe makampuni, lakini bahati mbaya sana sheria ile imepeleka mkono wake kutoza kodi kwa wananchi moja kwa moja, kwa wakulima moja kwa moja kwa hiyo kwa kweli ilikuwa ni usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii Bunge lako niliombe kwamba litoe shukrani kwa Serikali kwa hatua hii, maana yake Serikali ingeweza kukaa kimya na bado sisi tungeweza kulalamika na ingeweza kumaliza hata mwaka lakini haijamaliza hata miezi 6 tuemeweza kufuta hicho kipengela, kwa hiyo ni jambo la kushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha naye kwa kulichukua hilo na kulifanyia kazi, na nikupongeze na wewe kwa kulipokea hilo na kulifanyia kazi, na vile niwapongeze wajumbe wa kamati ya bajeti kwa kulifanyia kazi, hongera sana kwa kila Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna masuala yanayohusu miradi ya mikakati, na mradi mmoja wapo wa mkakati ambao tulisaini na wenzetu wa Uganda ni ule mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoyma, Uganda mpaka Chongeleani Tanga, huu ni mradi wa kimkakati na ni mradi ambao unabeba rasilimali yenye sifa za kidunia, na fadia zake kwa nchi yetu ni kubwa sana na hatua ambayo imechukuliwa ya kuleta marekebisho ambayo yanakwenda kuharakisha utekelezaji wa mradi huo ni ya manufaa makubwa sana kwa uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niipongeze Serikali kwa kukubaliana na kamati kufanya marekebisho ambayo yamefanywa ili kuweka jina halisi la mradi ule husika ambao baada ya mkataba ule kusainiwa na Serikali ulileta hapa bungeni ukawa *ratified* na sisi kwa kweli imekuwa jukumu letu kama wabunge kuhakikisha tunaiunga mkono Serikali kwa ajili ya maslahi ya watanzania wote kwa ujumla, kuhakikisha vikwazo ambavyo vingeweza kufanya mradi ule uweze kuchelewa. Kwa upande wa Tanzania tunaviondoa kwa haraka kupitia marekebisho ambayo yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimpongeze kila aliyeshiriki, nimpongeze kila Mbunge nikupongeze Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa hatua ambayo imefikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isipokuwa maoni yangu ya nyongeza nilikuwa nafikiri kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ananisikiliza hapa, nilikuwa nafikiri kwamba katika maandishi yale ya mwisho yaweke *time frame* kwamba yale tuliyoyaandika pale na kuyapitisha basi yaishie kwenye mwisho wa utekelezaji wa mradi isiwe kipengele kile kiachiwe tu kwa miaka 100 ijayo hapana, mradi utakapokamilika kutekelezwa basi iwe ndio mwisho wa kile kipengele ambacho tumekipitisha, zile *incentive* zote ambazo zinakuwa zimepitiswa. Nadhani hiyo ni kengele ya kwanza?

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia kwamba katika majadiliano ambayo yamefanyika ya kuondoa yale mapendekezo maengine mawili, yalikuwa ya msingi kabisa...

**SPIKA:** Huko kwa sababu hilo jambo halijaletwa humu, sio sehemu ya mjadala huu sasa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana, lakini nilikuwa napenda niseme kwamba mshikamano ambao umeonyeshwa kati ya...

**SPIKA:** Ahsante sana kama nia yako ni kujadili hilo...

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kuunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA:** Naomba tusubiri sana mpaka siku kikiletwa kitu kama hicho. Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana, kwa kunipa fursa hii kuchangia Muswada huu wa sheria wa dharura au *special Bill Miscellaneous Amendment.*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikupongeze wewe mwenyewe, nataka kuzungumzia kuhusiana na kifungu hichi cha 83(b), ambacho kinaondosha ile sheria iliyopishwa ya *withholding tax* kwenye mazao ya kilimo. Nilipouliza swali hili kutaka kujua ukweli kwa wakulima kwa sababu wakulima walikuwa wanalalamika wanatozwa kodi ya asilimia 2 na Serikali ilitujibu kweli inatoza hizo asilimia 2 kwa ajili ya sheria.

Mheshimiwa Spika, ulilisimamia hili ukaliona kwamba si sahihi, tunakushukuru sana na ulitaka mpaka kuipangua Kamati ya Bajeti ambayo kumbe nayo ilishatoa mapendekezo sheria hii isiwekwe kwa ajili ya kuwakata wakulima asilimia 2 ya *withholding tax*. Kwa hiyo, nakupongeza kwanza wewe kwa kulisimamia hili vizuri sana na mpaka leo Serikali imerudisha kwa dharura mswada huu ili kutoa kifungu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili nawapongeza pia kamati ya bajeti na wao kama ulivyowapongeza wamerudia na kuifanya kazi hii kwa haraka sana. Mchango wangu katika eneo hili mapendekezo yangu kwanza sisi kwenye tumbaku zao hili linajenga mjengeko wa bei mwezi wa pili, na tulipojenga mjengeko wa bei hii ambao unashirikisha wakulima, wadau lakini na wanunuzi, haikuweka kifungu ambacho au kipengele ambacho kitakuwa kinakatwa *withholding tax.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ilipokuja hii iliwanchanganya sana kwa sababu mauzo ya tumbaku yalianza mwezi wa 6 na wa 7 na wa 8, kwa hiyo

iliwachanganya sana wakulima na fedha zao mpaka sasa tunavyozungumza zimekuwa *withhold* na makampuni kwa mujibu wa sheria hii. Lakini isitoshe pia kwenye korosho mwezi wa kumi mnada uliopita nao pia wakulima wamekatwa hii *withholding tax* asilimia 2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu nilikuwa nataka kuona na hata kwenye pamba vile vile yamefanyika hayo makampuni ya *withholding* asilimia mbili. Ushauri wangu Mwanasheria Mkuu kama anaweza kuiandika vizuri kisheria kwamba kuanzia sheria hii inapopitishwa basi iwe imefuta pia toka ilipopitiswa ili wakulima hawa makampuni yarudishe fedha zao kwao, kwa sababu kwenye korosho leo hii mwezi wa kumi wameshafanya mnada, aliyeuza mwezi wa 10 amekatwa hii asilimia mbili lakini atakeuza mwezi wa 11,12 na Januari hatokatwa tutakapopitisha sheria hii, kwa hiyo italeta mtafaruk hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba sheria kama Mwanasheria Mkuu akiiweka kwamba kuanzia ilipopitishwa mie naichukulia kama ilipitishwa kimakosa kwa sababu kamati ya bajeti ilishauri sheria hii isiwekwe kifungu hiki lakini Serikali ilileta tukapitisha, sasa kuanzia tarehe hii ilopitiswa basi ifutwe na wakulima wale makampuni walio-*hold* fedha za wakulima ambazo mpaka saivi hawajawasilisha *TRA* na *TRA* ina *demand* zile fedha basi irudishe fedha zile kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ulikuwa ni huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipa na mimi niweze kuchangia huu mswada wa marekebisho ya sheria namba 6 kama ambavyo umewasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa

Serikali lakini pamoja na ushauri wa kamati wa bajeti kwa Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba tunashukuru sana Serikali sana sana kwa kukubaliana na kamati yetu kwa mapendekezo ambayo tuliyoshauriana nayo kwa muda mrefu na hadi tulipofikia hapo tulipofikia. Nataka nihakikishie Bunge lako kwamba Muswada huu umechambuliwa kikamilifu na utaleta tija kubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako leo linatuma salamu za furaha kubwa na sherehe kubwa kwa wafugaji wa nchi hii, kwa wavuvi wa nchi hii lakini kwa wakulima wa nchi hii, ilikuwa mzigo hii *withholding tax* asilimia 2 ilienda kukwaza sana kilimo ambacho kinachangamoto tayari kubwa nyingi, mifugo ambayo ina changamoto nyingi, shughuli za uvuvi ambazo zina changamoto nyingi, sasa ilipoletwa hii ilikwaza sana wananchi wetu ambao wanafanya kazi katika hili eneo, lakini hatimaye wewe mwenywe ulilionа mapema kamati iliona mapema, Bunge lako liliona mapema hatimae leo hii chini ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na mama yetu Samia Suluhu Hassan wameridhia na Bunge lako naamini litaridhia maamuzi haya kwa hiyo huu ni ushindi mkubwa na ni vizuri tukaenda namna hii hivi tunavyoenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa vipengele vile vingine vitatu vyote tumekubaliana vizuri mno na wenzetu, na hatuoni sababu tena ya kuzungumza chochote lakini baada ya vipengele kwa mfano sura ya tatu kurekebishwa na sura ya nne kuondoshwa kabisa, sheria sasa ilivyo hapa inabaki haina changamoto.

Mheshimiwa Spika, sasa labda ushauri mdogo katika eneo hili ni amejaribu kugusia na Makamu Mwenyekiti wa kamati ya bajeti, kwamba ni vizuri sana sasa tuwe tunafanya utafiri wa kina katika kuanzisha kodi zetu kuanzisha tozo zetu, tunapo taka kuanzisha tozo mpya tunapotaka kuanzisha kodi mpya ni muhimu sana tukafanya utafiti wa kina kabla hatujafanya hivyo, ili kuepuka changamoto kama hizi.

Kwamba mmemaliza kupitisha bajeti miezi mitano tu tayari leo mnagundua kasoro tena ni kasoro za kimapato ambapo wakati mwengine zinawalazimu kuzikagua ni mapato ambayo mlikuwa mmeyatabiria kuweza kuyakusanya katikati ya safari.

Mheshimiwa Spika, ushauri mdogo tu katika eneo hili amejaribu kugusia Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwamba ni vizuri sana sasa tuwe tunafanya utafiti wa kina katika kuanzisha kodi zetu, kuanzisha tozo zetu, tunapotaka kuanzisha tozo mpya, tunapotaka kuanzisha kodi mpya ni muhimu tukafanya utafiti wa kina kabla hatujafanya hivyo ili kuepuka changamoto kama hizi kwamba mmemaliza kupisha bajeti miezi mitano tu tayari leo mnagundua kasoro tena ni kasoro za kimapato ambapo wakati mwingine zinawalazima ku-*foregone* mapato ambayo mlikuwa mmeyakadiria kuweza kuyakusanya katikati ya safari, kumbe taasisi yetu ya utafiti iliyoko pale *TRA* kwa maana ya Kitengo cha Utafiti *TRA* kingekuwa kimeimarishwa vizuri kikawa na wataalam wengi wa kutosha na wakawa shirikishi, lakini pia hata pale Hazina, kile kitengo kinachoshughulika au idara inayoshughulika na mambo ya utafiti ingekuwa na yenyewe inafanya kwa kina, kwanza tusingekuwa tunabishana kirefu kwa sababu tungekuwa na ushahidi wa kila tunachotaka kukiamua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, ni muhimu sana kwanza kuimarisha hivi vitengo viimarishwe viwe vinafanya utafoti wa kina, lakini hii itatusaidia sana pia kwa sababu ni kwa muda mrefu sana mapato yetu hayaongezeki kwa kasi kama ambavyo tunakusudia. Mapato yetu hayaongezeki ukilinganisha na ukuaji wa uchumi, mapato yetu hayaongezeki ukilinganisha na mfumuko wa bei, mapato yetu hayaongezeki kulingana na sababu nyingine zile za kiuchumi tulizonazo. Kwa hiyo, kuna haja kubwa ya kufanya huu utafiti ambao utatuwezesha kuongeza mapato yetu kwa kiwango kikubwa pia, tutaepuka kuanzisha tozo na kodi ambazo zinapoanzishwa zinaleta mkanganyiko kwa wananchi wetu na kurudisha nyuma hata jitihada pia za kupiga maendeleo mbele.

Mheshimiwa Spika, pili ambalo naweza kushauri katika hili eneo ni suala la utafiti na tathmini ya misamaha inayotolewa. Kwanza ni kweli kabisa lazima tukubaliane kwamba, tunataka kupata misamaha katika maeneo mbalimbali, lakini pia tunataka kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba, misamaha yetu isizidi asilimia moja ya Pato la Taifa, hapo itatuwezesha kwenda vizuri zaidi na misamaha inayotolewa pia ni lazima iwanufaishe walengwa.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kwenye hotuba tu ya bajeti mnasema tumesamehe hili, tumesamehe hili, tumesamehe hili, lakini hakuna siku unaelezwa hiyo misamaha uliyoitoa imemnufaisha nani? Walengwa waliolengwa kwenye huo msamaha wamenufaika? Lakini Taifa pia limenufaika nini na msamaha unaotolewa? Kwa sababu, ni lazima tuwe na misamaha ambayo tunaweza kuipima na misamaha ambayo kweli tunathibitisha kwamba, huu msamaha tumeutoa kwa sababu hii. Sasa mwisho wa siku unaweza ukawa na misamaha ya kufurahisha watu tu, anapewa msamaha mwisho wa siku bidhaa mliyotegemea itashuka bei haikushuka bei, mnategemea kwamba, wananchi wale watanufaika kutokana na misamaha iliyotolewa na Bunge lao mwisho wa siku bei hazikushuka, sasa mnakuwa na misamaha ambayo ni ya kufurahisha kundi la watu, misamaha ambayo ni ya kufurahisha baadhi ya makampuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo mwaka jana katika bajeti hii ya mwaka 2021/2022 hapa tulipitisha tukasema kwamba, basi tukawatoze wale wakulima wa shairi *Withholding Tax* ya asilimia mbili, lakini wale wanywa pombe tuwasamehe kodi, matokeo yake hata wanywa pombe wenyewe pombe haikushuka bei pamoja na ile pombe inayotengenezwa kwa kutumia shairi na yenyewe haikushuka bei, kwa hiyo, unakuwa ni msamaha ambao umetolewa kufurahisha kundi la watu. Ni lazima kwamba, misamaha hii inayotolewa iwe *focused* na iwe kweli kwa manufaa ya Taifa. Tukiyazingatia haya na tukayafanya kwa usahihi na kwa ushirikiano mkubwa tunaweza kupiga hatua mbele sana

katika Taifa letu tukakusanya mapato mengi ya kutosha lakini na kuliwezesha Taifa letu kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tena kwa kusema naishukuru sana Serikali, nashukuru sana Waziri wa Fedha kwa kuwa msikivu sana. Daktari wa Uchumi kijana ambaye anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja na kuwahakikishia Wajumbe kwamba, Muswada tumeuchambua vizuri sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. Mheshimiwa Kwagilwa nilishakutaja utafutiwa na Mheshimiwa Tarimba Abbas, atafuata Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi nipate kuchangia Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na. (6) wa Mwaka 2021. Niungane na Wabunge wenzangu waliotangulia kuzungumza kuipongeza sana Serikali ya CCM kwa kuwajali wakulima, wafugaji na wavuvi, kuondoa *Withholding Tax* ya asilimia mbili katika mazao yanayotokana na shughuli hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa salamu hizo za pongezi, mimi nataka nichangie marekebisho ya ile *part three,* yaliyokuwa yameletwa kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Kodi. Sheria hii imefanyiwa marekebisho na sisi Kamati ya Bajeti tumeshauri sana ili kuondoa vikwazo vyote ambavyo vilikuwa vinakwamisha utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta. Sasa baada baada ya kuipitisha sheria hii hapa Bungeni na wenzetu wa Serikali kwenda kushirikiana na Serikali ya Uganda kuutekeleza mradi huu ninashauri mambo yafuatayo kwenye mradi huu:

Mheshimiwa Spika, mradi huu una gharama ya Dola Bilioni 3.5 karibia trilioni nane hivi. Tafsiri ya hii ni kwamba ni mradi mkubwa na ni fursa kubwa kwa wananchi wetu

ambako mradi unapita lakini na kwa Watanzania kwa ujumla. Kwa hiyo, basi ni lazima tuweke mikakati ya makusudi kuwawezesha wananchi wetu ambako mradi unapita ili washiriki kikamilifu kwenye shughuli zote kwenye fursa zote za ujenzi na uwepo wa mradi huu maeneo ambako bomba hili linapopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali za wananchi wetu tunazifahamu. Kikwazo kikubwa kwa wananchi wetu kushiriki kwenye fursa za bomba la mafuta hili ambalo tunalizungumzia itakuwa ni mitaji. Tayari Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii huko tunakotoka ambako bomba linapita wanawahamasisha wananchi wajiunge kwenye vikundi, lakini kikwazo kikubwa, ninarudia tena, kikwazo kikubwa ambacho kitawakumba wananchi wetu ni mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu sasa kwenye hili la kuwawezesha wananchi wetu mitaji ya kushiriki kwenye fursa za bomba la mafuta, ushauri wa kwanza ni kwamba kwa wale watakaofanikiwa kupata mikataba ya kazi kwenye bomba lile la mafuta kwa maana ya ama ku-*supply* vitu au kujenga, ninaomba kwamba ufanyike utaratibu maalum ili mikataba ile itumike kama dhamana kwenye mabenki. Kufanyike utaratibu maalum mikataba ile watakaokuwa wamepata itumike kama dhamana kwenye mabenki ili waweze kuchukua mikopo tena yenye riba nafuu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unajadili vizuri, lakini tujue kwamba, leo tunajadili sheria. Tunapojadili sheria ni tofauti kabisa na kujadili mada. Hatujadili bomba la mafuta na mambo yake, tunajadili sheria iliyoletwa hapa. Endelea tu Mheshimiwa tumalizie.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru. Kwa kuwa, umenipa na umeridhia niendelee naomba nimalizie vipengele vinavyofuata.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine kwenye bomba hili tunalokwenda kulijenga ni vyema Serikali ikalichukua kama

fursa na sisi kama nchi tutazame ushoroba kwa maana ya mkuza. *Corridor* hii ambayo tunakwenda kuijenga ya bomba la mafuta kutoka Hoima mpaka Chongoleani - Tanga siku zijazo tuifikirie kama fursa ya kupitisha bomba la gesi kutoka hapa gesi yetu ilipo ili tuweze kuipeleka mpaka Uganda na hatimaye Sudan ya Kusini na baadae Congo. Tuitazame kama fursa ya siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwenye hili bomba hili linapita kwenye Mikoa Nane na katika hiyo Mikoa Nane Mikoa ya mwisho huku kuelekea Bandari ya Tanga ni pamoja na Tanga yenyewe, Dodoma, Singida na Manyara. Sasa bomba hili litahitaji barabara ya kulihudumia hili bomba, barabara hiyo inayopita maeneo hayo ili kuweza kulifikia hili bomba kwa urahisi ni barabara ya Handeni – Kibilashi – Kiteto – Kondoa na Singida. Kwa hiyo, ni vyema Serikali inapofikiria kwenda kutekeleza mradi huu ifikirie pia kuitengeneza barabara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipatia muda na kuniruhusu kuchangia haya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba nilishakutaja.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada ulioletwa na Serikali unaohusiana na mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Namba (6), 2021 ambao umeletwa kwa ajili ya Wabunge tuweze kuubariki na kuwa sheria. Jambo la kwanza ningependa nichangie kwenye upande wa kile Kifungu 83(b) ambacho ni cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332.

Mheshimiwa Spika, ningeanza kusema yafuatayo. Kwanza jambo hili lilitaka lituponze Kamati ya Bajeti, laiti kama Serikali ingekuwa inaendeleza ule utulivu wake na usikivu wake wanapokutana na Kamati ya Bajeti yawezekana hata lile tatizo la kuweza kukusanya fedha hizi kuanzia mwezi wa

Julai, kama Mheshimiwa Vita alivyokuwa anazungumza, lingeweza kuepukika. Ninakimbilia niseme kwamba, katika siku zijazo Serikali inavyokutana kupata ushauri na Kamati ya Bajeti ningeomba sana wachukue ushauri ule na kuufanyia kazi, kwa sababu leo hii kuna watu waliumia kuanzia mwezi wa saba.

Mheshimiwa Spika, uelewe kilimo kinaajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania na hasa ukiondoa pengine asilimia tano ya wakulima wakubwa, waliobakia ni wakulima wa kawaida wadogowadogo ambao wengi sana ni *hand to mouth.* Sasa hii sheria ilivyokuwa imefanya kazi hakika iliwaumiza watu na bahati mbaya sana sheria haiwezi ikawa *retrospective,* lakini ningetamani kama ingekuwa inawezekana ikarudi nyuma kuweza kuwaokoa wale ambao waliweza kuchangia pasi na kuweza kujua kwamba sheria hii hakika ina kero kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naipongeza Serikali. Naipongeza kwa dhati kabisa Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuja na mapendekezo haya ambayo sasa mimi naona kama hatujachelewa ingawa wapo walioumia, lakini ninaamini mara baada ya Bunge lako Tukufu litakapopitisha mabadiliko haya Rais nae hatachelewa kuisaini ili sheria hii iweze kuanza kutumika mapema sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; Leo hii kwa marekebisho ya Sura ya 438, ile Sheria ya Usimamizi wa Kodi ambayo tunakwenda kuirekebisha sasa hivi inakamilisha hatma ya Serikali katika kuhakikisha zile *reliefs* ambazo zinahitajika kutokana na mkataba wa kati ya Tanzania na Uganda juu ya utengenezaji wa hili bomba la mafuta leo hii taratibu zile zinakwenda kukamilika. Kwa sababu tulishapitisha na kufanya marekebisho ya sheria nyingi sana, ilibakia *a fiscal reliefs* na leo inakwenda kukamilika na mimi naweza nikasema ninaunga mkono na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako la Tanzania liweze kukubali mabadiliko haya ambayo yamefanywa na Serikali ili sasa mradi huu muhimu ambao tumekuwa tukiusubiri na

tuliokuwa tukiugombania sana Tanzania na nchi nyingine uweze kwenda ukafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kama utaniruhusu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti alilizungumzia suala la *tax ombudsman* jambo hili linaleta ukakasi mkubwa sana kwa upande wa Serikali. Inawezekana isiwe ni *subject matter* ya majadiliano ya sasa hivi, lakini lina umuhimu kwa Taifa letu kwamba, kule katika *tax tribunal* kuna kesi nyingi yenye thamani ya zaidi ya trilioni 2.6 yamekwama. Ni nini ukakasi wa Serikali kuanzisha *tax ombudsman* ambapo ni sheria iliyoishapitishwa na Bunge lako Tukufu miaka mitatu imeshapita. Ni king'ang'anizi gani na uwoga gani wa kuanzisha hicho kitu?

Mheshimiwa Spika, Serikali tunachohitaji sisi ni mapato kwa ajili ya Taifa letu ili yaweze kwenda kusaidia shughuli nyingine nyingi sana. Trilioni 2.6 ni hela nyingi, hata kama tukizipata nusu kwa usuluhishi chini ya ofisi ya msuluhishi *tax ombudsman* yawezekana tukapiga hatua sana. Naiomba Serikali wakati itakapokuja kufanya *winding up* ya Muswada huu waweze kutugusia ni kitu gani kinachowafanya wakachelewa kiasi hiki kuweza kuanzisha ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas. Mheshimiwa Halima Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali, Namba (6) ya Mwaka 2021. Nikianza na Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Namba 332, *(The Income Tax Act)* ambayo pamoja na mambo mengine inafuta Kifungu cha 83(b) ambayo ilianzisha Kodi ya Zuio ya Asilimia Mbili.

Mheshimiwa Spika, naungana na wote ambao wametambua umuhimu wa kipengele hiki kufutwa, lakini siyo sifa sana pale Bunge linapotunga sheria halafu baada ya miezi minne Bunge hilohilo linakuja kurekebisha sheria, siyo sifa sana. Kamati ya Bajeti inayofanya kazi kwa niaba ya Bunge tuliliangalia hili jambo tukaelekeza Serikali namna ya kufanyia kazi, Serikali ikapiga chini lakini na Bunge letu sisi hapa, tuliwajibika na sisi kuangalia kwa kina ili tusimame imara kama Bunge kuzuwia sheria za namna hii.

Kwa hiyo, ninakiri kwamba, kuna uzembe kwa upande wa Serikali kutokufanya tafiti na kujua kwamba, tukianzisha kodi ipi, itakuwa na faida ipi, lakini vilevile na sisi kama Bunge tunatakiwa Kamati za kisekta ama Kamati mahususi zikileta mapendekezo tuyaangalie, tuyadadavue na tuyafanyie kazi kwa ufanisi kwa maslahi mapana ya wananchi tunaowawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na maoni ya Kamati ambayo yamependekeza, na ninaomba Serikali ilichukulie hili kwa umakini sana kwamba Serikali iimarishe vitengo vya utafiti.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nimpe Taarifa mchangiaji. Pamoja na mawazo mazuri na yeye ni Mjumbe wa Kamati, tunashauriana kuanzia kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, jambo hili kufika hatua hii Bunge halijafanya uzembe wala Serikali haijafanya uzembe, isipokuwa Mheshimiwa Rais aliona umuhimu wa kufanya jambo hili kwa sababu, katika majira haya sekta ya kilimo imepigwa na majanga mbalimbali yakiwemo mambo ya mbolea, yakiwemo mambo ya bei, akaona kwa sababu, sekta hii pia haikufaidika na fedha za *Covid* licha ya kwamba,

na sekta hii imeathiriwa na *Covid* basi iweze kupata nafuu ya kupunguza baadhi ya kodi ambazo zilikuwa zimekusudiwa kukusanya fedha na fedha hiyo ipatikane kutokea maeneo mengine ili wananchi waweze kupata nafuu.

Kwa hiyo, si kwamba, ni uzembe wa Serikali ama uzembe wa Bunge, bali ni huruma ya Mheshimiwa Rais kwamba kwa sababu tumeshapata fedha sehemu nyingine na sekta hii haikunufaika basi tuna sehemu ya kufidia fedha hii tuondoe hii kodi ambayo inaweka maumivu kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo, unapewa Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, siwezi kuipokea kwa sababu Rais ni kichwa kimoja, Bunge ni vichwa vya watu wengi tunaowakilisha wananchi. Ni jambo la aibu Mheshimiwa Mwigulu ukisema kwamba ni sahihi Bunge kupitisha kifungu ambacho ni kibovu na kukiri kwamba mpaka Rais akaone kifungu kibovu ndio alete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema *collective responsibility,* hata mimi ni Mjumbe wa Kamati, sasa ukitaka tuzungumze ya Kamati na wewe ulituambia nini na ulikuja kufanya nini, hatutaki kufika huko. Tunasema uwajibikaji wa pamoja sisi kama Bunge tulitakiwa tuwe na jicho la ziada ili mambo yasitokee. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa nazungumza suala la utafiti wa sera.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mwenye taarifa endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba uulinde muda wangu.

**SPIKA:** Muda ulindwe Katibu.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Halima Mdee kwamba kwa mujibu wa Ibara 63 Kifungu cha kwanza, Rais ni sehemu ya Bunge ikiwa nusu ya Bunge. Ukija kwenye sehemu ya pili, ndiyo inatoa madaraka sasa kwa Bunge kufanya kazi zake na sehemu ya tatu. Kwa hiyo, Rais kufanya *intervention* ni kitu ambacho ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Ahsante sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba niachane naye, kwa sababu nahisi ananipotezea muda.

**SPIKA:** Pokea taarifa hiyo Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, siwezi kuipokea kwa sababu hakuna popote kwenye Katiba ambako kumesema Rais ni nusu ya Bunge. Yeye ni sehemu ya Bunge kwa sababu tukitunga sheria ana nafasi yake ya ku-*assent* ile sheria ili iweze kufanyiwa kazi. Kwa hiyo, kila mmoja ana *role* yake *independently.* Kwa hiyo, tusichanganyane hapa.

Mheshimiwa Spika, suala la tafiti, nitasoma mambo kadhaa ili Serikali ielewe. Tumetolea mifano mbalimbali kwa ajili ya maeneo gani yanahitaji udharura, lakini kwa sababu ya suala la *research* tulipitisha Sheria ya Tozo hapa. Sasa ngoja nikusomee taarifa ya *TCRA* imesemaje? Kwa sababu tunapopitisha mapato, sisi tunafurahi Serikali wamefanya utafiti, kile ambacho Serikali ilikadiria kupata ipate ili huduma ziweze kupatikana. Serikali inapopitisha kodi, halafu kodi badala ya kuongezeka inapungua, tafsiri yake kulikuwa hakuna utafiti.

Mheshimiwa Spika, ngoja nikusomee, maana naona muda umeshaenda, wameshanipotezea muda. Uchambuzi wa miamala ya kifedha kwenye mitandao ya simu kabla na baada ya tozo, jumla ya miamala ya fedha imeshuka kwa

asilimia 12 kutoka shilingi milioni 352 mwezi Juni hadi shilingi milioni 307 mwezi Septemba baada ya tozo.

Mheshimiwa Spika, miamala inahusisha kutuma na kutoa fedha inaendelea kushuka wakati miamala isiyokuwa na tozo za Serikali inahusu malipo ya huduma inaendelea kupanda. Idadi ya miamala pamoja na tozo zimeendelea kupungua badala ya kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, uchambuzi wa miamala kifedha kwenye mitandao ya simu kabla ya tozo inatuambia, kuanzia...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima upokee taarifa kutoka kwa Waziri wa Nchi.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu kumpa taarifa Mheshimiwa Halima Mdee kwamba, nadhani amejisahau kidogo kwamba hoja tunayozungumza sasa ni marekebisho ya Muswada Maalum na una vifungu maalum ambavyo havitoi ufafanuzi na haviendani na Sheria ya Kodi ambayo ilizungumzia tozo katika miamala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu nimwamshe arudi kwenye hoja ambayo iko Mezani. Hiyo ya tozo za miamala tutakuja nayo siku nyingine kwa sababu hiyo ilishapita na shughuli zake zilishaanza kuendelea huko tulikotoka. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa...

**SPIKA:** Sijakuruhusu Mheshimiwa Halima. Umesikia taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi? Unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, mimi najadili uchambuzi uliofanywa na Kamati ya Bajeti, uchambuzi ambao umejadiliwa na Wabunge katika *context* ya kuishauri Serikali. Sasa aniache nimalizie tu, atulie. Unaogopa nini?

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Julai, 2020 tozo za miamala zilipoanza, jumla ya tozo zitokanazo na miamala ya fedha zimekuwa zikishuka kwa wastani wa 9% kwa mwezi kutoka shilingi bilioni 94 kwa mwezi Julai hiyo, mpaka shilingi bilioni 78 mwezi Septemba. Kodi zilizokuwa zinalipwa Serikalini kutoka kwenye mapato ya watoa huduma, zimeshuka kwa asilimia 39 kutoka wastani wa shilingi bilioni 28 kwa mwezi mpaka wastani wa shilingi bilioni 16 kwa mwezi. Mapato ya watoa huduma yameshuka kwa wastani wa 39% kutoka kwa wastani wa shilingi bilioni 88,500 mpaka…

**SPIKA:** Hizo *data* tumeshazisikia. Hoja yako nini yaani?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hoja yangu ni kwamba Serikali zingatieni ushauri wa Serikali kuimarisha vitengo vya utafiti wa Sera ya Mapato ili kuiwezesha Serikali kuwa na taarifa za uhakika. Siyo sifa kwenye suala hili la miamala tulitarajia kupata *1.3 trillion* tunakuja tunaambiwa utekelezaji wake Serikali inapata nusu.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Halima, huko kwingine kabisa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**SPIKA:** Utanipa taabu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, hapana, hapana. Namalizia. Nivumilie kama ulivyomvumilia Mheshimiwa Reuben.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Ndiyo. Kuna taarifa. Ooh, Mheshimiwa Waziri wa Habari na Teknolojia ya Habari.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kumpa taarifa msemaji. Taarifa anayoi-*cite* nilitamani sana aseme mwisho wa taarifa hiyo kwenye mjadala nini kilielezwa? Nayo ilikuwa kushuka kwa miamala hii ni jambo la kawaida kunapokuwa na *introduction* ya kodi mpya. Sasa naomba nimwambie, wakati tunaanza kukusanya tozo hii ya miamala anayoieleza, idadi ya miamala ilikuwa 12,330,223 na leo taarifa ya tarehe 27 mwezi wa Kumi, miamala ambayo ilirekodiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ni 13,489,119.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba apokee taarifa hii kwamba hili ni jambo la kawaida kwamba kuna kupanda na kushuka tunapokuwa na *introduction* ya kodi mpya. Ahsante.

**SPIKA:** Hivi sasa miamala iko juu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nilitarajia kwenye taarifa yake angeniambie miamala ilivyokuwa juu, *implication* yake ya kimapato kwa fedha ikoje? Ukinipa *story* za miamala kuwa mingi, inaweza ikawa mingi lakini wamefanya shilingi mbili mbili. Hizi ni *data* ambazo sisi tumepewa na wao wenyewe. Kama kampuni za simu zinazolipa kodi zinapata hasara kwa *39 percent*...

**SPIKA:** Mheshimiwa *data* zako zimeishia mwezi Septemba.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, hizi *data* tumepewa juzi kwenye Kamati.

**SPIKA:** Waziri amekupa *current.*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naona unamsaidia kujibu. Sisi tunaangalia hapa...

**SPIKA:** Ndiyo ukweli wenyewe, yaani umechagua ile miezi miwili ya mwanzo ile; mwezi wa Nane na wa Tisa ambapo huko ni kweli, lakini ungeendelea hadi sasa ambayo anakwambia Waziri, ni kwamba ilikuwa ime-*trip* chini sasa imerudi pale pale na imepanda juu hata ya pale ilipokuwa. Ndicho anachosema. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, tunazungumzia mapato. Kwa hiyo, ninachotaka anipe majibu kimapato, asinipe majibu kimiamala. Miamala inaweza ikawa mingi lakini isi-*reflect* mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme hivi kwa kumalizia; ushauri wa bure tu wa Kamati jamani, msini-*mind,* kwamba fanyeni utafiti kwa sababu siyo sifa, unatunga sheria leo halafu kesho; yaani tatizo unalitengeneza mwenyewe, halafu unataka uonekane kwamba wewe ni mkombozi kwenye hilo tatizo. Siyo sifa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tuvumiliane Mheshimiwa haya mambo yanahitaji ngozi ngumu tu. Ahsante sana. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbalii (Na. 6) wa Mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. Nakushukuru wewe mwenyewe pamoja na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuongoza Serikali na kuonyesha usikivu pamoja na wasaidizi wake; Mheshimiwa

Waziri wa Fedha, Mwanasheria Mkuu, Wizara ya Nishati na watendaji mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono hoja ambayo imewasilishwa na Serikali pamoja na maoni ya Kamati yetu. Hususan najielekeza kwenye mabadiliko ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, na hiki ambacho tunazungumza kufutwa kwa kifungu 83 (b). Kama nilivyotangulia kusema, naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali, naiomba kwa sababu hapa palikuwa na changamoto, Serikali inatambua yapo makampuni yanayonunua mazao kwa jumla ambayo yana tabia ya kwenye vitabu vyao vya fedha kuongeza kiwango kinachowalipa wakulima wakati kiuhalisia wanawalipa kidogo. Ndiyo maana kukawa na hiyo tafakuri ya nini kifanyike?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, kwa nia hiyo hiyo njema waliyonayo, waendelee kufanya utafiti, ni namna gani makampuni yanayonunua mazao ya wakulima iwe ya ufugaji au uvuvi, itaiwezesha Serikali kupata mapato ya kutosha na kuondoa upotoshwaji unaofanywa kwenye taarifa zao za fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nawashukuru wawakilishi wa vyama vya wavuvi, wafugaji na wakulima ambao walikuja kwenye kamati yetu kwa nyakati tofauti; na nikushukuru mwenyewe kwa kuridhia Muswada huu uje kwa hati ya dharura kwa maslahi ya Watanzania wetu ambao ambao wengi wapo katika sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niunge mkono mabadiliko yaliyowasilishwa na Serikali ya kurekebisha Kifungu cha 7 cha sheria ya usimamizi wa kodi, Sura ya 438 kwa kuongeza Kifungu cha 3 kwa nia ya kuhakikisha mradi huu wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda mpaka Chongoleani Tanga; nasi kama Kamati pamoja na Bunge lako hili tunatambua faida nyingi za mradi huu ikiwemo kuzalisha ajira 10,000, ikiwemo namna ambavyo Serikali

itapata mapato ya asilimia 40 kutokana na bomba hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Serikali itakusanya kodi kwa miaka 25 na hata umiliki wa hili bomba kupitia *TPDC.* Kwa hiyo, inaonesha utayari wa Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza ile miradi ya kimkakati. Katika hilo pia naishauri Serikali kwa kuwa inaendelea na majadiliano ya miradi mingine mikubwa mikubwa ikiwemo la kusindika gesi asilia Lindi, likiwemo la Liganga na Mchuchuma huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa spika, kwa hiyo, kama kuna vikwazo vyovyote katika hatua hizi za awali kwa masuala ya kikodi; na kwa sababu tunataka kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo, Kamati ya Bajeti kupitia ruhusa yako na kwa niaba ya Bunge, tupo tayari kuona miradi hii ya kimkakati ambayo ikitekelezeka vizuri itachangia pato la Taifa na kuwezesha sekta nyingine nazo kufanya kazi. Kwa hiyo, napongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati tumeshauri, kwa muktadha huo huo Serikali iangalie nayo sheria nyingine mbalimbali; kwa mfano tumezungumzia msamaha wa kodi. Tumeomba Serikali hebu ilitazame hususan katika sekta hii ya viwanda vya dawa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifungashio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulitupa ruksa ya kutembelea kiwanda cha dawa cha pekee hapa nchini cha Serikali kilichopo Keko. Katika ziara yetu ile tumegundua namna gani Serikali imeanza kufanya vizuri. Kiwanda kile sasa hivi kina uwezo wa kuzalisha dawa vidonge milioni sita tofauti na vidonge 1,500,000 lakini imeongeza uzalishaji wa dawa kutoka *Paracetamol* mpaka dawa zaidi ya 15. Hata hivyo, ina uwezo wa kuingia kwenye masoko ya Kimataifa yakiwemo soko la nchi za *SADC,* lakini changamoto ambayo walituomba ni Serikai kuangalia hii Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifungashio.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali itakapotathmini kodi mbalimbali, basi iweze kufanya na hilo ili tuweze kuisaidia hii sekta ya uzalishaji wa dawa hapa nchini, tuweze kujitosheleza na kupunguza gharama za uagizaji dawa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba nikushukuru sana. Naunga mkono, ahsante sana. Nampongeza tena Mheshimiwa Rais kwa hatua hii na kuwajali Watanzania ambao ndio wengi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa vile Waheshimiwa Wabunge wote tunakubaliana kwa kweli kimsingi na mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, basi namwomba Mheshimiwa Oran Njeza awe wa mwisho katika kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. ORAN NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Naipokea taarifa, sijui taarifa anapewa nani sasa?

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, ni Riziki Said Lulida... niliwahi kuingia hapa toka saa 8.00, lakini...

**SPIKA:** Ngoja kidogo. Nani anayeongea?

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, niko huku Msekwa.

**SPIKA:** Aah, Msekwa!

Mheshimiwa Spika, naona Mheshimiwa Njeza anakuwa wa mwisho. Hivyo natamani nami nichangie kwa vile ni namba moja, lakini kwa vile nimekaa huku, hujanitambua kama nipo hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spiuka, napenda kuwasilisha. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Bahati mbaya ambao hamtachangia mko wengi Mheshimiwa Lulida, ni pamoja na wewe. Ninayo orodha ndefu hapa, lakini sasa Mheshimiwa Njeza atakuwa wa mwisho ndiyo ruling yenyewe. Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe. Wewe hii hoja uliiona kwa macho mwenyewe, baada ya kuiona, yote haya yametokea. Nami nianze kwa kukushukuru wewe. Kwa hiyo, ilianzie hapa Bungeni, kuna Mbunge akauliza hilo swali na kweli hii imewaumiza sana wananchi.

Mheshimiwa Spika, hii 2%, siyo tu ilikuwa inawaumiza wakulima, lakini hizi ni kodi ambazo zinasababisha mazao yetu yatoroshwe kupelekwa nchi jirani. Kuna ushahidi mkubwa kuwa hata kahawa, pareto na mahindi kwa kiasi kikubwa wananchi wamekuwa wanatorosha kwa ajili ya kodi zetu wakati mwingine ambazo zinaonekana ni mzigo sana kwa wananchi. Naishukuru sana Serikali kwa hii hatua, namshukuru vile vile Mheshimiwa Rais kwa hatua aliyochukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya marekebisho kwenye *Tax Administration Act* (Na. 7), hii ni muhimu sana tena sana kwa sababu, itatuwezesha na sisi kama nchi Tanzania Pamoja na hii ya sasa hivi ambayo imerekebishwa, kutambua kuwa maeneo ambayo tunaweza kuwa na *double tax agreements* yanaweza kuwa na manufaa makubwa sana kwa nchi yetu na isiishie hapa tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali iangalie namna gani iboreshe eneo hili ili ikiwezekana tuangalie *double tax agreements* ambazo sasa hivi zinaonekana kwa muda mrefu hatujaingia nazo, nazo ziwe sehemu ya hili eneo ambalo ni *section seven* ya hii *tax administration*.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, tena sana. Kwa haya, nami naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa twende upande wa Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa hoja hii imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge, sitakuwa na mengi ya kusema. Labda moja tu ambalo nilitaka niwape *assurance* Waheshimiwa Wabunge ni hili ambalo wameulizia kuhusu uanzishwaji wa Ofisi ya Msuluhishi wa Masuala ya Kikodi.

Leo hii hivi tunavyoongea, Katibu Mkuu Kiongozi pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ambaye ndiye Mlipaji Mkuu, pamoja na timu ya ngazi ya Makatibu Wakuu, baadhi ambao walikuwa na masuala yanayohusu miundo kama hiyo, walikuwa na kikao ambacho bado kinaendelea kwa ajili ya kupitisha muundo ambao uta-*fit in* jambo hili ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisemea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliona nilisemee hili kuwapa *assurance* kwamba siyo jambo ambalo lilikuwa limesimama isipokuwa lilikuwa bado linafuata taratibu za kiutawala, baada ya kupitishwa sheria ingehitajika kutengenezwe muundo ili liweze ku-*fit in* kwenye muundo na hicho ndicho ambacho leo kikao hicho kilikuwa kinafanyika kwa ajili ya kupitisha muundo na baada ya muundo kupitishwa basi zitafuata taratibu za masuala mengine ya *human resource* ili ofisi iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lakni jambo lingine ambalo ningependa nilifafanue, alisema ndugu yangu kwamba tulitoza kwenye mazao halafu tukasamehe pombe. Hatujasamehe pombe, isipokuwa katika majira haya ya *slow down* ya kiuchumi, kuna maeneo kwenye *sectors* tulisema tu tusipandishe. Siyo kwamba tumesamehe, tulisema tusipandishe kwa ajili ya kuzingatia kwamba kama dunia nzima uchumi ulikuwa ume-*slow down*, ukiendelea kupandisha kodi unaweza uka-*discourage* zaidi *production*.

Kwa hiyo, hayo ndiyo baadhi ya maeneo ambayo tulikuwa tumeyaangalia.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wote watashuhudia na lenyewe niliwekee tu kumbukumbu, Serikali inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan ni Serikali inayosikiliza sana. Hata Wizara tulipoenda kukaa na Kamati ukienda kwenye *Hansard* za Kamati wakati wa Bunge la Bajeti hata wenyewe walikiri kwamba kwa kweli tumesikilizwa na karibu kila hoja tulisikilizana. Kwa hiyo niliona na yenyewe hii niiweke sawa isije ikaonekana kama Serikali tunakuwa hatusikilizi.

Mheshimiwa Spika, tunapokea sana ushauri wa Kamati zetu na si kwa Wizara ya Fedha tu, bali kwa Wizara zote, tunapokea sana ushauri wa Kamati zetu na sisi tutaendelea kupokea na kufanyia kazi kama ambavyo matakwa ya sheria yanataka, lakini pia na ushirikiano ambao tunapata kutoka kwa Kamati zetu. Tunajenga nchi moja na hizi tulizonazo ni dhamana tu na kila mmoja hapa ana dhamana kufuatana na mipaka hiyo ya dhamana inavyosema . Kwa maana hiyo, ujenzi wa nchi unatutegemea tu sote na tutaendelea kuyapokea maoni na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba pia Kamati imekuwa ya msaada sana katika masuala mengi tu. Ikitokea kuna jambo tumeliweka na ukahitajika ulazima wa kuliangalia hizo ni *dynamics,* unaweza ukaangalia sasa hivi mambo yanavyoenda yanabadilika kwa haraka haraka sana. Kwa hiyo, hizi *dynamics* ni sehemu ya kusikiliza ushauri na ni sehemu ya Serikali kuwa sikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuhahakikishie kwamba kwa kwenda na usikivu huu huu, tutasababisha wananchi wetu kule wapige hatua kubwa sana za kimaendeleo kuliko kuwa *rigid* katika mambo ambayo uzito wa hoja umeshauona ila ukatae tu, kwa sababu utaonekana ume-*create* tatizo na kurudi kutafuta suluhisho. Nadhani kufanya uharaka huu ndiyo kupata suluhisho la haraka ambalo linaweza likatufanya

tukatengeneza maendeleo na tukatengeneza fursa kwa ukubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ilitolewa hoja ya kuhusu utekelezaji wa upande wa sheria ambao *AG* atajibu, lakini kwetu sisi utekelezaji wa hii ambayo itakuwa imepita, tutakaa na Wizara zote ambazo zimeguswa, tuone utekelezaji wake tunaenda nao namna gani. Tutakaa na Wizara zote zikiwemo Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Viwanda pamoja na *Local Governments* ambao kwa namna moja ama nyingine tutalazimika kushauriana katika baadhi ya maeneo kuhusu *smooth transition* ya utekelezaji wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aje hapa mbele, atuhitimishie hoja yake. Karibu sana Mheshimiwa *AG,* Dkt. Feleshi, tafadhali. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana tena kwa kunipa hii nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala huu wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba Muswada huu umepata jumla ya wachangiaji 10 ambao wamepata fursa kupitia kiti chako ambao ni Mheshimiwa Omari Kigua ambaye pia ni Makamu wa Kamati ya ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Mheshimiwa Joseph G. Kakunda, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Njeza pamoja na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ambaye pia ni Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni faraja kwamba wachangiaji wote wameunga mkono hoja na ningependa kujibu. Kulikuwa na hoja hasa iliyoletwa na Mheshimiwa Kakunda kuhusu ukomo wa kutumika kwa kifungu cha 7(3) niombe tu kujibu kwamba kwa mujibu wa masharti sasa kifungu hicho kilichoongezwa uhai wake na ukomo wake unaendana na mradi uliotajwa kwenye sheria hiyo. Kwa hiyo ndiyo maana ni mradi mahsusi umetajwa kwenye kifungu hicho na kifungu hicho hakitatumika kubeba mradi mwingine isipokuwa kwa masharti ya kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni ile iliyowasilishwa na Mheshimiwa Vita Kawawa ambaye yeye alikuwa anaongelea ni lini hasa mabadiliko haya yatatumika. Awali ya yote labda nieleze kwamba alieleza dhana ya kamati jinsi ilivyokuwa imewasilisha hoja kwenye bunge lililopita. Ningependa tu kusema kwamba baada ya Kamati ya Bajeti kufanya mawasilisho yake baadaye Bunge lilikaa kupitia kifungu kimoja baada ya kingine na mwisho lilihoji na ule Muswada ukapitishwa kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kifungu kile ni halali mpaka sasa kwa sababu kilipitishwa na Bunge hili kwa mujibu wa taratibu za utungaji wa sheria. Kwa hiyo sasa baada ya majadiliano haya nafikiri kuna hatua mbili zinakuja endapo Bunge litapitisha sasa mabadiliko yanayopendekezwa na baadaye Muswada huu kupitishwa kuwa Sheria kwa hatua zote na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa mujibu wa sheria ya tafsiri ya Sheria Sura ya kwanza sheria hii itaanza kutumika mara tu baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo naomba tu nirudie kuwashukuru sana wote ambao wamechangia na wengine ambao hawakuchangia na kwa niaba ya Serikali niwahakikishie tu kwamba Serikali tutaendelea kupokea maoni na kutoa ufafanuzi wa maeneo mengine mtambuka kwa sababu ndiyo wajibu wetu kuhakikisha kwamba sheria zinazopitishwa na Bunge hili zinafikia malengo yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Halima Mdee awe na amani tu, baada ya miezi minne kupita baadaye yamekuja mabadiliko haya, kwa kuwa yamekuja kwa kufuata zile taratibu za kisheria na ni kwa manufaa ya Watanzania na Wabunge kama tunavyojua kwa mujibu wa Katiba ni wawakilishi wa wananchi, kwa hiyo sheria inayotarajiwa nafikiri itawasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa niruhusu niombe kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO*:*** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuhitimisha hoja yako vizuri na kwa kifupi. Hoja imetolewa na imeungwa mkono nashukuru sana sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Bunge Zima.

**SPIKA:** Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.6 Bill, 2021)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Sehemu ya Nne imefutwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Katibu endelea.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Mheshimiwa mtoa hoja, nakuomba sasa utoe taarifa ya kazi iliyofanyika na kisha utoe hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2020, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 6 wa Mwaka 2021*(The Written Law Miscellaneous Amendments No.6 Bill, 2021)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.6 wa Mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous*

*Amendments) No.6 Bill, 2021)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuwa sasa ametoa hoja ya kwamba, Bunge tukubali kuupitisha Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali No.6 wa mwaka 2021. Sasa wajibu wa kiti hapa ni kuwahoji Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka 2021 (The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 6 Bill, 2021 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote kabisa wameafiki Muswada huu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI**:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Tatu kwa lengo la kuondoa upungufu ambao yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo. *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to keep the Law updated with some challenges observed in its implementation)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa natangaza rasmi kwamba Muswada huu umepita katika Bunge letu katika hatua zake zote na sasa safari ya Muswada huu ni kwenda mbele ya Mheshimiwa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ili akitoa kibali chake basi iwe sheria kamili ya nchi.

Kwa hiyo nitumie nafasi hii kumpongeza sana mtoa hoja, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Dkt. Feleshi, lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na wale wengine wote ambao wamehusika na jambo hili wakiwepo wataalam wetu na watu wote kwa kweli tunashukuru sana sana kwa mabadiliko haya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia kwamba jambo hili lirudi hapa na kama mlivyochangia ninyi wenyewe na mlivyoona. Wabunge wetu wengi bado ni wapya, lakini sasa upya unazidi kwisha na mfano huu wa sheria hii imekuwa ni funzo mojawapo kwetu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Nafikiri siku moja mlisikia nilisema hii ilipita wapi hii, watu wakanishambulia, wakanishambulia kwenye mitandao na wapi? Nilisema kutoka moyoni bahati mbaya mimi sijui huwa nikoje, yaani kitu kama kina tatizo huwa nasema pale pale, yaani ni shida kidogo, muwe mnanivumilia.

Natoa maoni yangu pale pale kwa sababu vitu vingine vinataka hapo hapo. Nia ni njema, mtu atakayenichunguza mimi huwa na nia njema tu na kwa roho nyeupe, sisemi kitu kwa nia yoyote ile ambayo ni mbaya. *(Makofi)*

Tulisema Bunge hili linaenda kuwangalia wakulima kipekee, hili Bunge la Kumi na Mbili na katika kuangalia wakulima na ndiyo maana nikashtuka hii ilipita wapi kwa sababu sisi tumesema, tutasimama na wakulima wa nchi hii. Sasa hii ilipitapitaje hii!

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka na tunachojifunza hapa ni kwamba, Kamati iwe ya Bajeti au Kamati nyingine yoyote kama kuna jambo ambalo mnatofauti hamkuelewana na Serikali kule, lakini ninyi mnaamini ni *fundamental* hilo jambo, kwanza mnapaswa kumwambia Spika ili aje akijua. *(Makofi)*

Haya yalipokuwa yanakuja Kamati ya Bajeti kwa sababu ya vikao vingi, Spika hakujua wala aliyekaa kitini

wakati ule wa kupitisha *Finance Bill* na sikuwepo wakati huo, walikuwa wengine, kwa hiyo kitu kinapita kwa sababu anayesoma anasoma tu kawaida. *(Makofi)*

Inatakiwa Spika apate taarifa ili amwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali waliangalie vizuri zaidi jambo hilo ambalo Kamati ina-*feel* kabisa kwamba hili liangaliwe. La pili, kwa wale wa Chama Tawala jambo la namna hiyo linapaswa kurudi kwenye *Caucus*, lile ambalo kuna tofauti kubwa kati ya Kamati na Serikali, ndivyo Mabunge yote yanavyoendeshwa, ili litoke kwenye *caucus* lije hapa, ninyi wenyewe mseme wakulima wapigwe kodi kutoka kwenye *Caucus* ambacho naamini kule hamtakubali. Mkikubali kazi kwenu, mnanielewa, ndiyo maana ya kuwa Mbunge yaani vitu unavyovifanya, unabeba na *responsibility* yake.

La tatu, anayekuja kusoma ile taarifa ikibidi labda hilo halikufanyika la *Caucus* na kadhalika. Anayesoma ile taarifa aisome kwa kurudia hata mara tatu kipengele kile ambacho hamkukubaliana. Katika hili Kamati hatukukubaliana na Waziri, lakini Waziri ameng'ang'ania kuleta hapa sisi Kamati tunasema kabisa Mheshimiwa Spika, hili hatukulikubali na madhara yake ni haya, haya na haya. Kitu cha namna hiyo hakipiti. Kwa sababu Wabunge lazima msimame na Kamati yenu kwa sababu kamati ile imefanya kazi kwa niaba yenu na inawaeleza jambo hili si jema, madhara yake ni haya sasa nyie mtapitishaje, itakuwa vigumu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana katika taratibu za Kibunge mambo ni vizuri yakaishia nje ya Ukumbi wa Bunge kwa taratibu tulizonazo hapa inakuwa tu ni mahali pa kurekebisha hapa na pale kwa tofauti ndogo ndogo ambazo tunamwomba Mwanasheria Mkuu au Waziri au nini, bwana sheria hii hapa, vile vitu vidogo vidogo labda ingesomeka hivi, labda hiki kimezidi hivi, naye anaangalia, wanashauriana, wanakubali au wanakataa na kadhalika. Yale mambo yote ambayo ni *fundamental* ni lazima kule na ikibidi kama nilivyoeleza, hizo ndiyo taratibu zetu za msomaji, msomaji naye kama mnaona jambo lina utata, hamlikubali, mnamchagua na msomaji, kuna ufundi wa kusoma pia, lazima tukubaliane,

msomaji ambaye atakuja kuwasilisha hoja hasa, vizuri. *(Makofi)*

Hata hivyo, kwa hili kwa kweli tunawapongeza Serikali, tunampongeza sana Rais wetu kwa sababu asingekubali yeye lisingerudi na kwenye bajeti ijayo lingetusumbua sana hili, lazima Waziri wa Fedha angepata tabu sana. Hivyo, hili lingebadilika tu, kwa sababu sisi tunawawakilisha wakulima na lazima tuwalinde wakulima wetu, wapo katika hali ngumu na tunataka tukuze kilimo, wanataka wabakiwe na kitu kidogo, halafu watumbukize tena kwenye kilimo, kilimo kiweze kukua.

Kwa hiyo, nawapongeza sana wote, kuanzia Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, sisi Wabunge wote kwa nia hii njema kwa wakulima wetu. Kwa kweli ni habari nzuri sana inayoenda kuwasaidia vya kutosha.

Kwa kuwa sasa kazi yetu imekamilika, kuna tangazo tu la semina ya kesho pale Msekwa ambayo itaanza muda wa kawaida wa saa tatu inayohusu masuala ya mitaala ya elimu nchini, nitawaomba sana nyote mfike mapema ili tuweze kuwasikia wenzetu katika Wizara ya Elimu watakuwa wanatueleza nini. Naomba sana tuwahi Waheshimiwa.

Tangazo la pili linahusu jarida la Bunge; kwamba kuna jarida, kila baada ya Mkutano tunatoa jarida, hili ni jarida la Mkutano wa Nne wa Bunge, kwa hiyo ni vyema tukaondoka nalo, linahusu shughuli za Mkutano wa Nne. Tunakupongeza sana Katibu kwa kuandaa jarida hili na aendelee na la Mkutano wa Tano.

Kesho tutakuwa tunahitimisha shughuli zetu hapa ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atasoma hotuba kesho jioni ya kuahirisha Bunge. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuwahi, kwa sababu hatutakuwa na ratiba ndefu yoyote na wale ambao wanakuwa Msekwa kesho wote tuwe humu ndani ili kwa pamoja tuweze kumsikiliza Mheshimiwa

Waziri Mkuu na yale ambayo Serikali itakuwa inatueleza kwa kesho.

Kwa hatua hiyo basi, shughuli za leo zote zimekamilika na tumemaliza mapema kidogo, imekuwa ni jambo jema. Basi naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa11.20 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 12 Novemba, 2021 Saa Nane Mchana)*